SportPesa
TZS. 482,274,020
CHEZA USHINDE JACKPOT
SPORTPESA.CO.TZ | PIGA *150*87#
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



**Waandishi** wa IPP wang'ara tena uandishi habari EJAT

UKURASA 3


# Nipashe

Jumamosi Septemba 11, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0580700

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




**Hatima ya Dembele mbioni kuamuliwa**

UKURASA 20



Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, akiwa chini ya ulinzi wa askari Magereza, baada ya kuwasili katika Mahakama Kuu ya Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi, mkoani Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Mbowe awakana makomando

• **Ni** washtakiwa wenzake kesi ya uhujumu, nao pia wadai hawamfahamu... *Endelea ukurasa wa 2*



Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Taifa, Rais Samia Suluhu Hassan, akiongoza kikao cha Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM Ikulu Chamwino, jijini Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

## DED wa Gairo asimamishwa kazi tuhuma wizi wa mabati

UKURASA 3



Gwajima



Silaa

## Hatima ya Gwajima, Silaa CCM yaiva

UKURASA 2

**MICHEZO** **SIMBA, YANGA DES. 11 LIGI KUU** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

HABARI KITAIFA

# Mbowe awakana makomando

Na Kulwa Mzee

MWENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, amewakana washtakiwa wenzake watatu waliokuwa makomando wa Jeshi la Wananchi Tanzania (JWTZ) Kikosi 92 KJ, huku nao wakidai kuwa hawamfahamu.

Licha ya kuwakana na wao kumkana, washtakiwa wote wamekana mashtaka ya kesi ya ugaidi wanayoshtakiwa ikiwamo kula njama kufanya ugaidi na kumsababishia majeraha aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya.

Hata hivyo, makomando hao wamekiri kufahamiana kwa madai walikuwa wanafanya kazi pamoja Kikosi cha Makomando Ngerengere.

Hayo yalibainika jana Mahakama Kuu Divisheni ya Makosa ya Rushwa na Uhujumu Uchumi wakati washtakiwa wakijibu mashtaka yanayowakabili na kusomewa maelezo ya awali.

Washtakiwa walijibu mashtaka mbele ya Jaji Mustapha Siyani, huku Jamhuri ikiwakilishwa na Wakili wa Serikali Mwandamizi, Robert Kidando, Nassoro Katuga, Ignas Mwinuka, Esther Martin na Wakili wa Serikali Tilimanyo Majigo na Jenitreza Kitali.

Upande wa utetezi unawakilishwa na Wakili Peter Kibatala, John Mallya, Jebra Kambole, Sisty Aloyce, Nashon Mkungu, Michael Mwangasa, Alex Maseba, Faraja Mangula, Dickson Matata, Evaresta Kisanga na Hadija Aron.

Washtakiwa katika kesi hiyo ni Mbowe, makomando Halfan Bwire, Adam Kasekwa, maarufu Adamu na Mohamed Ling'wenya, ambao wanakabiliwa na mashtaka sita.

Inadaiwa katika shtaka la kwanza, washtakiwa wote, walikula njama kati ya Mei Mosi na Agosti Mosi 2020 katika Hoteli ya Aishi iliyopo Manispaa ya Moshi mkoani Kilimanjaro na maeneo mbalimbali ya Jiji la Dar es Salaam, Morogoro na Arusha, kulipua vituo vya mafuta, hivyo kuhatarisha usalama wa taifa na kusababisha hofu kwa jamii.

Katika shtaka la pili, wote wanadaiwa kula njama kufanya vitendo vya kigaidi na kutaka kumsababishia majeraha Ole Sabaya.

Shtaka la tatu, Mbowe anadaiwa katika kipindi hicho na mahali hapo alitoa Sh. 600,099 ili kuwawezesha Halfani, Adamu na Ling'wenya huku akiamini fedha hizo zitasaidia katika kufanya ugaidi kwa kulipua vituo mbalimbali vya mafuta na mikusanyiko kwa lengo la kuharibu misingi ya kisiasa, katiba, uchumi na sifa ya Tanzania.

Shtaka la nne wanadaiwa kushiriki vikao vya kufanya vitendo vya kigaidi wakati shtaka la tano, mshtakiwa Adamu anadaiwa Agosti 5, mwaka 2020, eneo la Rau alikutwa na bastora yenye namba A 5340 aina ya Luger.

Mshtakiwa Halfani katika shtaka la sita anadaiwa Agosti 10, 2020, kwa lengo la kuhatarisha usalama wa nchi, alitumia sare za JWTZ na Jeshi la kujenga Taifa (JKT) ambazo ni suruali moja ya JKT, pamoja na suruali nne za JWTZ, fulana moja, koti la moja, jaketi, kofia tano, overall tano, begi la kubebea vifaa vya JWTZ lijulikanalo kwa jina la ponjoo, vyeo vinne vya koplo, mikanda minne, soksi jozi moja, sweta, begi la mafunzo ya parachuti, kibuyu cha kunywea maji pamoja na kisu aina ya AK 47 CCCP, vyote vya JWTZ.

Washtakiwa wote kwa mara ya kwanza walikana mashtaka yanayowakabili, upande wa Jamhuri uliomba kuwasomea maelezo ya awali.

Wakili Kidando alidai mshtakiwa wa kwanza hadi watatu waliajiriwa na JWT, walifuzu mafunzo ya ukomando na walikuwa kikosi cha 92 KJ, Ngerengere mkoani Morogoro.

Alidai washtakiwa wanadaiwa kula njama, kufanya vikao kwa ajili ya kufanya ugaidi, Mbowe anadaiwa kutoa fedha za kufadhili na Julai 2020 alimwomba Luteni Urio amtafutie makomandoo ili wamsaidie kutekeleza ugaidi ikiwamo kusababisha majeraha kwa viongozi wa serikali na kulipua vituo vya mafuta na masoko.

Anadai Mbowe alitoa Sh. 600,099 kufadhili washtakiwa wenzake, mshtakiwa 2 na 3 walikamatwa wakiwa katika harakati za kumsababishia majeraha Sabaya na Mawasiliano kati ya Urio na Mbowe yalifanyika kwa njia ya telegrams.

Walipotakiwa kujibu, mshtakiwa wa kwanza, wa pili na wa tatu walikubali taarifa zao binafsi yakiwamo majina yao, walikuwa wanajeshi, makomando Kikosi cha 92 KJ Ngerengere, walifukuzwa kazi kwa madai ya utovu wa nidhamu, wote walikutana kazini lakini walikana maelezo mengine ya mashtaka ikiwemo kumfahamu Mbowe.

Mshtakiwa Mbowe alikubali taarifa zake binafsi ikiwamo ni Mwenyekiti wa CHADEMA, lakini alikana maelezo yote ya mashtaka ya ugaidi ikiwamo kuwafahamu mshtakiwa 1, 2 na 3.

Wakili wa Serikali Mwandamizi, Esther Martin, alidai upande wa Jamhuri unatarajia kuwa na mashahidi 24 na vielelezo 19. Wakati utetezi ulidai utaleta mashahidi 11.



Spika wa Bunge, Job Ndugai, akimwapisha Dk. Stergomena Tax, kuwa Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, bungeni jijini Dodoma jana, baada ya kuteuliwa na Rais Samia Suluhu Hassan. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Samia amteua Dk. Tax kuwa mbunge

Na Mwandishi Wetu

RAIS Samia Suluhu Hassan, amemteua Dk. Stergomena Tax kuwa mbunge katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Dk. Tax alikula kiapo cha utii jana bungeni kwa ajili ya kutumikia nafasi hiyo mbele ya Spika wa Bunge, Job Ndugai.

Taarifa iliyotolewa jana na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais Ikulu, ilisema uteuzi wa Dk. Tax ulianza jana na ameteuliwa kutoka katika nafasi 10 za Rais kwa mujibu wa Katiba.

Kabla ya uteuzi huo, Dk. Tax ambaye ana shahada ya uzamivu katika uchumi, alikuwa Katibu Mtendaji wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) kuanzia mwaka 2013 hadi Agosti, mwaka huu.

Dk. Tax amewahi kushika nafasi mbalimbali serikalini zikiwamo Naibu Katibu Mkuu iliyokuwa Wizara ya Uchumi na Mipango mwaka 2006 hadi 2007, Katibu Mkuu Wizara ya Viwanda na Biashara mwaka 2007 hadi 2008 na Katibu Mkuu iliyokuwa Wizara ya Ushirikiano wa Afrika Mashariki mwaka 2008 hadi 2013.

Pia aliwahi kuwa Ofisa Mtendaji Mkuu wa Mkakati wa Kuboresha Mazingira ya Biashara Tanzania (MKUMBITA).

Kielimu, Tax alihitimu shahada ya kwanza ya uchumi katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam mwaka 1991 na baadaye kujiunga na Chuo Kikuu cha Tsukuba na kuhitimu shahada ya umahiri ya falsafa (M. Phil) na baadaye shahada ya uzamivu (Ph.D) katika masuala ya usimamizi sera na maendeleo ya uchumi.

# Hatima ya Gwajima, Silaa CCM yaiva

Na Augusta Njoji, DODOMA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), kimesema kimepokea taarifa kutoka Kamati ya Maadili ya Wabunge wa chama hicho, kuhusu tuhuma zinazowakabili wabunge watatu waliohojiwa na kamati hiyo hivi karibuni kwa ajili ya kufanya uamuzi.

Wabunge hao ni Josephat Gwajima (Kawe), Jerry Silaa wa Ukonga na Mbunge wa Kuteuliwa, Humphrey Polepole.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC), Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka, alisema CCM ni chama ambacho kina misingi na uendeshaji wake ni Katiba, Kanuni na taratibu.

"Niwahakikishe kwamba CCM bado ipo imara hasa katika kulinda na kuhakikisha kwamba inaendeleza msingi wake wa kuwapo kwake. Ni kweli kamati ya wabunge imeshakabidhi taarifa kwa chama lazima nikiri na hatua zinazofuata ni taratibu ndani ya chama chetu.

"Hiyo ilikuwa hatua ya awali, hatua ya pili mpaka tunafikia kwenye kufanya maamuzi (uamuzi). Chama kinaheshimu sana misingi ya kuanzishwa kwake kwa kufuata katiba, kanuni na taratibu," alisema.

Alifafanua kuwa katika kanuni za uongozi za CCM, suala hilo likipokewa na chama linaenda Kamati ya Usalama na Maadili.

"Likitoka hapo ndani ya chama chetu linategemea na hoja ambayo ipo na inatakiwa kwenda ngazi gani. Ikitoka kamati ya maadili kuna Kamati Kuu (CC) kuna yale mashauri ambayo yanakwenda NEC kwa ajili ya uamuzi," alisema.

Alisema kama lipo jambo la aina hiyo ambalo linahusu kufikishwa kwenye vikao vya uamuzi muda ukifika watasema.

"Tunakiri kupokea taarifa ya wabunge na hatua inayofuata ni mapema kusema lakini tumepokea tunaendelea na utaratibu kwa mujibu wa katiba na kanuni zetu," alisema.

Awali, akitoa taarifa kuhusu kikao cha Kamati Kuu ya CCM iliyokutana jana chini ya Mwenyekiti wake, Rais Samia Suluhu Hassan, alisema kimewapitisha wagombea wa CCM katika uchaguzi mdogo utakaofanyika hivi karibuni kwenye jimbo la Ushetu na Konde.

Aliwataja waliopitishwa kuwa ni Emmanuel Cherehani (Ushetu) na Mbarouk Amru Habibu (Konde) na kampeni za CCM zitaanza Septemba 25, mwaka huu, ambapo Katibu Mkuu Daniel Chongolo atazindua kampeni hizo kwa Jimbo la Ushetu.

Aidha, alisema kamati hiyo imempongeza Rais Samia na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, kwa kufanya kazi ya kuwaletea Watanzania maendeleo.

HABARI KITAIFA

# DED Gairo asimamishwa kazi tuhuma wizi mabati

**Patson Andugalile na Beatrice Inyasi,** TUDARCo

WAZIRI wa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu, amemsimamisha kazi Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Gairo, Asajile Mwambambale, kutokana na tuhuma za wizi wa mabati 1,172.

Tukio hilo lilitokea wakati akiwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Kilosa kabla ya kuhamishiwa Gairo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa juzi kwa vyombo vya habari na Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano serikalini TAMISEMI, Nteghenjwa Hosseah, walipokea taarifa ya maandishi kutoka kwa Mkuu wa Mkoa wa Morogoro, ikibainisha kuna upotevu wa mabati 1,172 uliotokea Agosti 17, mwaka huu, kwenye bohari ya Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa.

Taarifa hiyo iliweka wazi kuwa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Morogoro kwa kushirikiana na vyombo vya ulinzi na usalama, imefanikisha kupatikana kwa mabati hayo na yameshapelekwa kwenye maeneo husika na ujenzi wa madarasa unaendelea. "Katibu Tawala wa Mikoa wa Morogoro alishamwelekeza Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa kuwachukulia hatua za kinidhamu watumishi wanne walio chini yake waliohusika na upotevu huo," alisema Hossea katika taarifa hiyo.

Aidha, Waziri Mwalimu aliwakumbusha watumishi wote wa sekretarieti za Mkoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kufanya kazi kwa weledi, kuwa waadilifu na makini katika utendaji kazi wao wa kila siku.

Upotevu wa mabati hayo ulitokea Agosti 17, mwaka huu, katika Bohari ya Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa.



Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani Mkoa wa Arusha, Solomon Mwangamilo, akiwaelekeza wanafunzi namna ya kuvuka barabara kwa uangalifu, jijini humo jana. **PICHA: TUMAINI MAFIE**

# MNH yanunua mashine kusaidia tiba corona

**Na Mary Geofrey**

HOSPITALI ya Taifa ya Muhimbili (MNH) imenunua mashine mbili maalum (Spectra Optia) zitakazosaidia kutoa tiba ya magonjwa zaidi ya 10 ikiwamo UVIKO-19 na upandikizaji uloto.

Mashine hizo zenye thamani ya Sh. milioni 245 zitasaidia kuvuna chembechembe mama za kuzalisha damu (haematopoietic stem cells), mazao ya damu ikiwamo chembe sahani (platelets), chembe nyeupe (granulocytes) na Utegili (Plasma).

Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Damu na Mkuu wa Kitengo cha Magonjwa ya Damu MNH, Stella Rwezaula, alisema jana jijini Dar es Salaam kuwa mashine hizo zinaingia kwa mara ya kwanza nchini.

Alisema kwa wagonjwa wa corona, zinamsaidia kufyonza sumu iliyopo kwenye mwili wa mgonjwa aliyezidiwa na kumsaidia kupatiwa tiba ifanye kazi kwa haraka na kupona.

"Wale ambao wapo kwenye hatari zaidi ya corona unaweza kumweka kwenye hizi mashine na kuondoa sumu na kemikali katika mwili wa mgonjwa akapata nafuu na kuendelea na matibabu ya kawaida," alisema Dk. Rwezaula na kuongeza kusema kwa wagonjwa wenye saratani watapandikizwa uloto katika hospitali hiyo.

Alisema wataanza kuchuja chembe za uloto na kuanza kupandikiza nchini kwa mara ya kwanza, huduma ambayo haipo Afrika ya Mashariki.

Kuhusu uchangiaji damu alisema mashine hizo zinasaidia kupunguza idadi ya wachangiaji wa damu kwa mgonjwa mmoja kutoka sita hadi 12 na kuwa mchangaji mmoja.

Pia alisema mashine hizo zinamsaidia mtu kuchangia tena baada ya wiki mbili, tofauti na mfumo wa zamani wa uchangiaji ulilazimu kuchangia tena baada ya miezi mitatu hadi minne.

"Ukilinganisha na uchangiaji damu wa kawaida, mgonjwa anachangia damu baada ya miezi mitatu hadi minne kulingana na jinsia yake.

"Hii ni kwa sababu katika uchangiaji wa kawaida unachukua mazao yote ya damu kwa mara moja, wakati mashine inachukua tu zao la damu linalohitajika na damu yote kumrudia mchangiaji, ndiyo maana unaweza kumrudia mchangiaji huyo baada ya wiki mbili kuchangia tena kwa mazao yote ya damu," alisisitiza.

Alisema mazao hayo ya damu baada ya kuvunwa, yatatumika kwa wagonjwa mbalimbali kama tiba hususani kwa magonjwa wenye upungufu wa chembe sahani, chembe nyekundu na chembe nyeupe ambazo hawana.

Dk. Rwezaula pia alisema wenye tatizo la damu kushindwa kuganda kwa sababu tofauti watapewa Utegili (Plasma).

Alisema mashine hizo pia zinaweza kutoa matibabu kwa wagonjwa wenye selimundu kubadilisha damu na kuwekewa damu isiyokuwa na selimundu ili kuondoa athari mbalimbali za selimundu kama kiharusi.

Alitaja wagonjwa wengine watakaonufaika na mashine hizo kuwa ni wenye matatizo ambao wanaweza kubadilishwa utegili (Plasma), kama wagonjwa waliopooza, ulegevu wa misuli na magonjwa mengine.

Kwa upande wake, Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Damu, Elineema Meda, alisema wagonjwa walilazimika kwenda nje ya nchi kupata huduma ambapo iliwagharimu zaidi ya Sh. milioni 200 hadi 250, lakini nchini huduma hiyo itapatikana kwa Sh. milioni 70 hadi 80.

# Waandishi IPP wang'ara tuzo za EJAT

**Na Waandishi Wetu**

WAANDISHI wa Habari 12 wa IPP wameng'ara katika tuzo za Umahiri wa Uandishi wa Habari Tanzania (EJAT) kwa mwaka 2020 ambazo huratibiwa na Baraza la Habari Tanzania (MCT).

Katika tuzo hizo ambazo zilitolewa jana na MCT, waandishi wa habari wa IPP kupitia magazeti ya Nipashe na The Guardian walishika nafasi ya kwanza na ya pili katika vipengele mbalimbali vilivyokuwa vikiwaniwa.

Mshindi wa jumla katika tuzo hizo mwaka 2020 ni Adrian Mgaya kutoka Mlimani TV. Wengine waliochuana naye katika nafasi hiyo walikuwa ni Sanula Athanas (Mhariri wa Habari wa Nipashe), Veronica Mrema (Maisha na Matukio) na Lasteck Mushi (Habari Leo).

Sanula ameshinda tuzo tatu katika vipengele tofauti ambavyo ni Habari za Elimu na kingine kinachohusu Utalii na Uhifadhi kote ameshika nafasi ya kwanza, ya pili na ya tatu na tuzo ya Haki za Binadamu na Utawala Bora amekuwa mshindi wa kwanza.

Wengine walioshinda ni Elizabeth Zaya aliyeibuka mshindi wa kwanza katika tuzo za Habari za Uchunguzi, Mpigapicha Bora ni Jumanne Juma, Mchora Katuni Bora mshindi ni David Chikoko ambaye amechukua nafasi ya kwanza na ya tatu huku Muhidini Msamba akichukua nafasi ya pili.

Katika kundi la tuzo ya Jinsia na Watoto, mshindi wa pili ni Henry Mwangonde (The Guardian) na wa tatu ni Elizabeth Zaya na Habari za Afya mshindi wa tatu ni Christina Mwakangale.

Kundi la tuzo za Habari za Usalama Barabarani aliyeibuka katika eneo hilo ni Augusta Njoji, ambaye amekuwa mshindi wa kwanza na upande wa Hedhi Salama mshindi ni Renatha Msungu ambaye naye ameibuka mshindi wa kwanza.

Kundi la Wazi, mshindi wa kwanza ni Mary Geofrey na wa pili ni Jenifer Gilla, wote kutoka Nipashe. Wengine ni Zuwena Shame (The Guardian) ambaye ameshika nafasi ya pili tuzo ya Kilimo na Biashara ya Kilimo.

Katika tuzo hizo, mtoto Khadija Sadiki (13) aliibuka kuwa mshindi wa tatu katika tuzo ya Uandishi wa Habari za Ubunifu na Maendeleo ambaye kazi zake zilirushwa na DW Swahili.

Awali, akizungumza katika tuzo hizo, Waziri Mkuu mstaafu, Jaji Joseph Warioba, alivitaka vyombo vya habari nchini kujikita katika kuandika habari zinazowagusa wananchi na kuibua hoja ambazo zitaleta mjadala wa kuliekeza taifa kwenye maendeleo.

Jaji Warioba ambaye alizindua tuzo za EJAT mwaka 2021, alisema vyombo vingi vya habari vimeegemea katika kutoa maelezo kuhusu viongozi wa serikali na kiwasahau wananchi hususan wa vijijini ambako kuna matatizo zaidi.

Alisema tasnia ya habari imekua hivi sasa hususani katika kipindi cha miezi michache na kwamba juhudi ziongezwe katika kuandika habari zilizojikita kwenye utafiti wa maendeleo ya taifa.

**Imeandaliwa na Romana Mallya na Christina Mwakangale**

# Msuya astaafu ARU baada ya miaka 14

**Na Joseph Mwendapole**

MKUU wa Chuo Kikuu cha Ardhi (ARU), aliyetumikia chuo hicho kwa miaka 14, Cleopa Msuya, amestaafu rasmi.

Msuya ambaye aliwahi kuwa Waziri Mkuu na Makamu wa Rais, amekabidhi rasmi uongozi kwa Mkuu wa Chuo Mteule, Jaji Mkuu mstaafu Mohammed Chande, katika hafla fupi ya makabidhiano hayo ilifanyika jana chuoni hapo.

Akizungumza baada ya kukabidhi nafasi hiyo, Msuya alitaka vyuo vikuu kuzingatia malengo ya uanzishwaji wake.

Msuya alisema baadhi ya vyuo kikiwamo Chuo Kikuu cha Ardhi, vilianzishwa kwa lengo la kusaidia juhudi za serikali kuhakikisha vijana wengi wa kitanzania wanapata elimu kutokana na serikali kuwekeza katika kujenga shule nyingi kwenye kila kata.

Alisema shule hizo zimejengwa ili vijana wengi wanaomaliza darasa la saba waendelee na elimu ya sekondari ndiyo sababu ya kupanua wigo wa vyuo vikuu na vya kati ili vijana hao wajiendeleze na elimu ya juu.

Msuya aliitaka ARU kuendelea kujitafakari kuhusu kupanua wigo wa fani mbalimbali ili kutekeleza azma ya uanzishwaji wa chuo wa kudahili vijana wengi zaidi.

Pia Msuya alisifu aina ya ufundishaji wa Chuo Kikuu cha Ardhi kwamba unatoa wahitimu wanaoweza kupambana na soko la ajira kwa kiasi kikubwa ikilinganishwa na wahitimu kutoka vyuo vingine. "Nawapongeza sana Chuo Kikuu cha Ardhi kwa kuandaa vijana waliopikwa vyema wanaoweza kupambana na soko la ajira. Hii ni tofauti kubwa sana na vyuo vingine," alisema Msuya.

Naye Jaji Mkuu mstaafu Chande alimshukuru Rais Samia Suluhu Hassan kwa kumpa dhamana ya kukisimamia na kushauri chuo hicho akiwa Mkuu wa Chuo wa pili tangu kilipoanzishwa mwaka 2007.

Alisema atashirikiana vyema na watendaji wakuu pamoja na mihimili mingine yaani Baraza la Chuo pamoja na Seneti katika kushauri namana bora ya kuleta ustawi mzuri wa chuo kwa maslahi ya taifa. Chande alisema uzoefu alioupata katika kufanya kazi kwenye maeneo ya ushauri na usimamizi wa sera katika taasisi zingine za elimu ya juu ndani na nje vitasaidia katika kutekeleza majukumu yake kwa kipindi chote atakachokua kwenye nafasi hiyo.

Naye Mwenyeketi wa Baraza la Chuo, Prof. Costa Ricky Mahalu na Makamu Mkuu wa Chuo, Prof. Evaristo Liwa, kwa nyakati tofauti, walimshukuru Msuya kwa kuongoza chuo kwa kipindi chote cha miaka 14.

# Marekani yaisaidia Tanzania kupambana corona

**Na Patson Andugalile, TUDARCo**

SERIKALI ya Marekani kupitia Shirika la Maendeleo la Kimataifa (USAID), imezindua mradi wa kuimarisha usimamizi wa matibabu ya wagonjwa wa corona katika hospitali za rufani za mikoa.

Taarifa iliyotolewa kwa vyombo vya habari jana na Ubalozi wa Marekani ilisema hadi sasa USAID limewekeza Dola milioni 25.1 za Kimarekani katika maeneo hayo.

Ilibainisha kuwa mradi huo wenye thamani ya dola 750,000 za Kimarekani, utatekelezwa katika hospitali nne za rufani za mkoa ya Dodoma, Tanga (Bombo), Arusha (Mount Meru) na Mwanza (Sekou Toure).

Utekelezaji wake kwa mujibu wa taarifa hiyo, utafanywa na shirika la kuhudumia watoto wanaoishi katika mazingira magumu la Save the Children, ambalo litasaidia utoaji wa vifaa vya tiba ya gesi ya oksijeni na mafunzo kwa watoa huduma za afya.

Mengine ni mafunzo yatazingatia matumizi sahihi na utunzaji wa vifaa hivi ili kutoa huduma bora na kupanua wigo kwa wagonjwa wa corona wenye shida ya mfumo wa upumuaji ambayo yatajumuisha uandaaji na usambazaji wa miongozo kazini iliyohidhinishwa kitaifa, na ufuatiliaji wa tiba ya oksijeni baada ya kuondoka kwa wakufunzi. Taarifa hiyo ilibainisha kuwa mradi huo unakusudia kuhakikisha vituo vya afya vinatoa huduma bora kwa wagonjwa wote wa corona wenye uhitaji maalum kwa lengo kuimarisha afya zao kwa uharaka.

Aidha, mradi huo utaimarisha uwezo wa watoa huduma katika kuhudumia wagonjwa hao kwa ufanisi na ubora katika kutoa huduma endelevu za corona.

"UVIKO-19 (corona) ni janga la dharura la dunia lililokuja na changamoto nyingi zisizotarajiwa na zinzaobadilika kila wakati katika sekta ya afya. Serikali ya Marekani imeamua kufanya kazi bega kwa bega na Tanzania kwa kusaidia mpango wake wa kitaifa wa kukabiliana na janga la UVIKO-19," ilibainisha taarifa hiyo.

Taarifa hiyo ilisema Marekani itashirikiana na wadau wote sekta ya afya Tanzania kupunguza athari zinazotokana na janga hilo katika kuhakikisha afya na usalama wa jamii nzima.

"Pamoja na kupunguza athari za janga hilo kwa jamii, upatikanaji sawa na utoaji wa chanjo za UVIKO-19, kupunguza athari za ugonjwa na vifo vitokanayo na UVIKO-19, USAID pia litasaidia kuzuia na kupunguza athari za UVIKO-19 kwenye miradi ya VVU/UKIMWI na wanufaika wake.

Akizungumza katika uzinduzi wa mradi huo, mtaalamu na msimamizi wa miradi ya USAID, Dk. Miriam Kombe, alisema: "Msaada huu ni pamoja na kupunguza athari za janga hilo kwa jamii, upatikanaji sawa na utoaji wa chanjo za UVIKO-19, kupunguza magonjwa na vifo vitokanavyo na UVIKO-19 na kuzuia na kupunguza athari za UVIKO-19 kwenye programu zetu za usaidizi ya UKIMWI na walengwa."

"Janga la UVIKO-19 ni miongoni mwa changamoto kubwa kwa afya, ustawi, na usalama wa kiuchumi kwa jamii nzima. Lazima tushirikiane kulishughulikia kwa haraka," alisema.

Uzinduzi huo ulihudhuriwa na Mkurugenzi wa Masuala ya dharura na utayari, Dk. Elias Kwesi, na Mganga Mkuu wa Serikali, Dk. Aifello Sichalwe.



Mkuu wa Chuo Kikuu cha Ardhi (ARU), Jaji Mkuu mstaafu Mohammed Chande Othman, akizungumza wakati akikabidhiwa ofisi na mkuu wa chuo hicho aliyemaliza muda wake, Waziri Mkuu mstaafu David Cleopa Msuya, wakati wa hafla iliyofanyika chuoni hapo juzi. **PICHA: MPIGA PICHA WETU**

# Mvutano waibuka ujenzi hospitali ya wilaya

**Na Thobias Mwanakatwe**

UJENZI wa Hospitali ya Wilaya ya Momba mkoani Songwe ambao utagharimu zaidi ya Sh. milioni 900 umeibua mvutano kuhusu eneo gani ijengwe huku ushauri wa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) ukipuuzwa.

Katika mvutano huo, Mbunge wa Momba, Condester Sichalwe, amesema wananchi wa jimbo hilo wanataka ijenge katika kijiji cha Makamba, Kata ya Chitete, lakini baadhi ya viongozi wa serikali ya wilaya, mkoa na halmashauri, wanataka ijengwe katika eneo la Tindingoma.

Akizungumza na gazeti hili jana, Sichalwe alisema hakubaliani na wazo la kutaka hospitali hiyo ijengwe eneo la Tindingoma kwa sababu itakuwa ikiwalazimu wananchi kutembea umbali mrefu kufuata huduma za matibabu kuliko ambavyo ingejengwa Makamba.

"Hospitali ikijengwa katika kijiji cha Makamba itawarahisishia wananchi wote kupata huduma za matibabu kwa sababu iko karibu na kata zote 14 za Halmashauri ya Wilaya ya Momba tofauti na eneo la Tindingoma ambalo liko jirani na kata moja iliyoko jirani na Halmashauri ya Wilaya ya Mbozi," alisema.

Sichalwe alizitaja kata ambazo wananchi wake watafaidika kupata huduma kwa ukaribu sana iwapo hospitali hiyo itajengwa katika kijiji cha Makamba kuwa ni Nkangamo, Ndalambo, Nzoka, Myunga, Ikana, Kamsamba, Mpapa, Mkulwe, Chilulumo, Chitete na Msangano.

Katika kuweka msisitizo wa kutaka hospitali hiyo ijengwe Makamba, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Ummy Mwalimu, alimwandikia barua yenye kum Na. AH 161/164/01/118 ya Agosti 18, mwaka huu, Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Omary Mgumba, akitoa maelekezo ijengwe katika kijiji cha Makamba.

"Nimepokea barua ya Julai 6, 2021 kutoka kwa Mhe. Condester Sichalwe Mbunge wa Momba akiwasilisha ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri ya Wilaya ya Momba. Hata hivyo naelekeza kuwa kifanyike kikao cha Baraza la Madiwani ili kuridhia ujenzi wa hospitali hiyo katika kijiji cha Makamba ili wananchi waweze kupata huduma kwa ukaribu," ilieleza barua ya waziri ambayo tumeiona.

Pamoja na maelekezo yaliyotolewa na waziri, kikao cha Baraza la Madiwani kilichofanyika Agosti 27, mwaka huu, kilipitisha ujenzi wa hospitali hiyo kufanyika Tindingoma badala ya Makamba.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Momba, Mathew Chikoti, akizungumza na gazeti hili kwa simu jana, alisema maelekezo ya waziri hayakuwa ya kuamuru ujenzi wa hospitali hiyo ufanyike kijiji cha Makamba bali alitoa maelekezo kifanyike kikao cha Baraza la Madiwani ndicho kitoe uamuzi.

Chikoti ambaye ni Diwani wa Mkulwe, alisema sababu iliyofanya ujenzi wa hospitali isijengwe katika kijiji cha Makamba ni eneo la kijiji hicho kujaa maji hivyo haliwezi kustahimili majengo ya ghorofa.

# Matatani tuhuma uchomaji makanisa

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

JESHI la Polisi mkoani Ruvuma, linawashikilia watu wanne, wakazi wa eneo la mtaa wa Namanyigu, Manispaa ya Songea, kwa tuhuma za kuchoma moto maeneo mawili ya makanisa ya Pentecoste na Calvary na kusababisha uharibifu wa mali zenye thamani ya Sh. milioni mbili.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Ruvuma, Joseph Konyo, alisema matukio hayo yalitokea Septemba 6, mwaka huu, majira ya saa 11:00 alfajiri katika eneo la Mtaa wa Namanyigu.

Alisema katika tukio la kwanza, makanisa mawili yalichomwa moto kwa wakati mmoja na kwamba moto huo haukusababisha madhara kwa binadamu, lakini uharibifu wa baadhi ya mali zenye thamani ya Sh. milioni mbili zikiwamo samani na vitabu vya Bibilia ambavyo vilikuwa vimehifadhiwa ndani ya makanisa hayo.

Konyo alisema baada ya kutokea tukio hilo, Jeshi la Polisi lilifuatilia na kubaini kuwa maeneo yote mawili ya makanisa yaliyochomwa moto, yanamilikiwa na watu binafsi. Alisema Kanisa la Pentekoste linamilikiwa na Mchungaji Alfred Milanzi na la Calvary linamilikiwa na Peter Msemwa.

Alisema ufuatiliaji katika ofisi ya mipango miji Manispaa ya Songea ulibaini makanisa hayo yako katika viwanja namba 225 na 1276 kwenye mtaa wa Namanyigu Mshangano na yamejengwa katika viwanja ambavyo havijawahi kumilikishwa kwa mwananchi yeyote.

Kuhusu matumizi ya viwanja hivyo, alisema inaonyesha ni kwa ajili ya makazi ya watu kwa mujibu wa mchoro wa mipango miji namba ulioandaliwa kwenye eneo hilo la kuabudia la Pentecoste lililoko kwenye chanzo cha maji lilipimwa na kupewa namba 1276.

Alisema mmoja wa wanafamilia, George Nchimbi, alithibitisha kuwa eneo hilo linatumika kwa kanisa la Pentekoste ni chanzo cha maji na kwamba eneo ambalo serikali ya mtaa ilikwisha litenga kama chanzo cha maji alipatwa na mshangao baada ya kuona mmoja wa wanafamilia ya Nchimbi ameliuza eneo hilo kwa watu wawili tofauti.

Kamanda Konyo alisema kuwa katika eneo la kuabudia la kanisa la Calvary, upelelezi wa polisi umebaini kuwa eneo hilo limejengwa kwenye kiwanja namba 225 ambalo walipangishwa na Mourus Lungu na kwamba lilijengwa bila kibali kwa kuwa baada ya kufuatilia mipango miji, imebainika ni kwa ajili ya makazi ya watu na si kanisa.

# NEC yataka wasimamizi wa uchaguzi kushirikisha vyama

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) imewaagiza wasimamizi wa uchaguzi ngazi ya majimbo na kata zinazotarajia kufanya uchaguzi mdogo Oktoba 9, mwaka huu, kushirikisha vyama vyote vya siasa ili uwe huru na haki.

Kamishna wa NEC, Jaji mstaafu Mary Lougway, alitoa agizo hilo wakati akifungua mafunzo kwa wasimamizi na wasimamizi wasaidizi wa uchaguzi katika majimbo ya Konde (Zanzibar) na Ushetu (Shinyanga) pamoja kata 10 kutoka majimbo mbalimbali ya Tanzania Bara.

Jaji Longway alisema uchaguzi ni mchakato unaojumuisha hatua na taratibu zinazopaswa kufuatwa na kuzingatiwa kwa kuwa ndio msingi wa uchaguzi kuwa mzuri, wenye ufanisi na kusaidia kuondoa malalamiko au vurugu wakati wa uchaguzi.

Alisema jambo muhimu wanalotakiwa kuzingatia wasimamizi hao ni kujiamini na kufanya kazi kwa weledi na kuzingatia katiba, sheria za uchaguzi, kanuni, maadili ya uchaguzi na maelekezo ya tume. Pia aliwataka kufanya utambuzi wa vituo vya uchaguzi mapema kwa lengo la kuhakikisha mpangilio mzuri, utakaoruhusu uchaguzi kufanyika kwa utulivu na amani.

Hata hivyo, alionya wasimamizi hao wa uchaguzi kuachana na udugu na upendeleo kwa ndugu na jamaa, ambao hawana sifa za kufanya shughuli za uchaguzi na badala yake waajiri watendaji wa vituo wenye weledi na wanaojitambua kadri inavyowezekana.

Naye Msimamizi wa Uchaguzi wa Jimbo la Mwanga mkoani Kilimanjaro, Mwajuma Nasombe, alisema mafunzo hayo yatawajengea uwezo wa kusimamia uchaguzi, demokrasia katika masuala ya uchaguzi kwa kushirikisha wadau wengine ili uchaguzi uwe wa huru na haki.



Wafanyabiashara wa vitunguu wakivisafisha wakati wakisubiri wateja katika Soko la Urafiki maarufu kama 'Mahakama ya Ndizi', jijini Dar es Salaam jana. Kilo moja ya vitunguu inauzwa kwa bei ya 1,200/-. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Waitara ataka magari ya mawaziri yatozwe faini

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mwita Waitara, ameagiza kituo cha usimamizi wa mizani cha Nala, jijini Dodoma kuyatoza faini magari ya mizigo inayozidi uzito bila kujali kama gari husika ni la waziri au kiongozi yeyote.

Waitara pia ameagiza kituo hiko kuacha kuwatesa abiria kwakuwaweka kwa muda mrefu pindi mabasi yanapokamatwa badala wayaruhusu huku sheria zingine zikifuatwa.

Kauli ya Naibu Waziri Waitara imekuja baada ya wafanyakazi wa kituo hiko kudai kumekuwa na baadhi ya magari yakikamatwa yanadai ni viongozi wa serikali ili kukwepa faini likiwamo gari la mchanga lililopigwa faini ya Sh. milioni 38 kutokana na mzigo kuzidi.

Waitara aliyasema hayo wakati wa ziara ya kikazi ya kukagua kituo hiko baada ya kupokea malalamiko kutoka kwa wananchi juu ya urasimu unaofanywa katika mizani.

"Ninaomba viongozi wa serikali magari yao yapigwe faini kama magari ya raia wa kawaida kwa sababu ile ni sheria na imewekwa ili kila mmoja aifuate. Hata likiwa gari langu wewe piga faini tu," alisema Waitara.

Alisema gari likizidi uzito wa mzigo linachangia kikubwa kuharibu barabara ambayo inatengenezwa kwa gharama kubwa tofauti na mzigo uliobebwa.

Faini anayopigwa raia wa kawaida, alisema ndiyo anayotakiwa kupigwa kiongozi yeyote wa serikali na akikataa wawasilishe jina lake wizarani ili hatua za kisheria zichukuliwe dhidi yake.

"Mfano mzuri ni huyu dereva Abdul Kapumba amekaa hapa na amepigwa faini ya zaidi ya Sh. milioni tano sasa kwa nini viongozi wasipigwe faini? Serikali haihitaji kuona barabara zinaharibiwa na magari ya mizigo ilhali sheria ya upakiaji mizigo ipo," alisema Waitara.

**UKAMATAJI MABASI YA ABIRIA**

Waitara aliwataka wafanyakazi wa kituo hiko kuhakikisha wakikamata mabasi wasiwatese abiria kukaa kwa muda mrefu, badala yake wakibaini kosa waliachie basi liende na wao wafuate sheria za kuwalipisha faini wenye basi husika.

"Naomba hili mlizingatie sana nyie wafanyakazi wa vituo vya mizani kwa sababu nimekuwa nikipokea malalamiko mengi ya wasafiri wakidai wanawekwa kituoni kwa muda mrefu kwa kosa la basi na sio wao abiria," alisema Waitara.

Hata hivyo, Waitara aliwataka wananchi kutokubali kujazwa katika basi na wakikaribia kituo cha mizani wanavushwa na Hiace ili kwenda kupandia mbele, jambo alilosema wanahatarisha maisha yao wenyewe.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Kila la kheri wawakilishi wetu michuano ya CAF

**WAWAKILISHI** wengine wa Tanzania Bara kwenye michuano ya kimataifa; Azam FC na Yanga, watashuka dimbani leo na kesho katika viwanja tofauti kuipeperusha bendera ya nchi baada ya jana Biashara United kubeba jukumu hilo kwa kuvaana na Dikhil ya Djibouti kwenye Kombe la Shirikisho Afrika.

Biashara yenyewe ilianzia ugenini nchini Djibouti wakati Azam FC ambayo nayo inaiwakilisha nchi kwenye Kombe la Shirikisho Afrika, leo majira ya saa 1:00 usiku ikitarajiwa kuikaribisha Horseed FC ya Somali katika Uwanja wao wa Azam Complex uliopo Chamazi, Dar es Salaam.

Kwa upande wa Yanga inayoiwakilisha nchi kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, kesho itashuka Uwanja wa Benjamin Mkapa majira ya saa 10: 00 jioni kuikaribisha Rivers United ya Nigeria katika mechi ya awali ya mashindano hayo yanayoongoza kwa utajiri mkubwa kwa ngazi ya klabu Afrika.

Tukiachana na matokeo iliyoyapata Biashara United, jana, macho yote ya mashabiki wa soka nchini na Watanzania kwa ujumla, sasa yanaelekezwa kwa Azam FC leo na Yanga kesho, kila mmoja hususan wapenda maendeleo ya mpira wa miguu nchini akitaka kuona zinapata ushindi wa kishindo ili kurahisisha kazi kwenye mechi za marudiano mwishoni mwa wiki ijayo.

Ndiyo, tunaamini hivyo kwa kuwa Nipashe ni mdau namba moja wa sekta ya michezo nchini, kwa mantiki hiyo daima malengo yetu nikuona soka kama ilivyo michezo mingine ikipiga hatua kuanzia ile inayoshirikisha mchezaji mmoja mmoja, klabu hadi timu za taifa.

Tunafahamu kama mchezaji yeyote ama klabu atapata/itapata matokeo chanya pamoja na sifa kuelekezwa kwao, lakini bado itajenga heshima kubwa kwa soka la Tanzania kwa ujumla na kuzidi kupandisha viwango kuanzia ngazi ya klabu hadi nchi kwa mchezo husika.

Wote tunatambua kwamba hadi Tanzania inafikia hatua ya kuingiza timu nne kwenye michuano ya kimataifa, ilitokana na Klabu ya Simba kufanya vizuri kwa kufika hatua ya robo fainali kwenye Ligi ya Mabingwa kuanzia msimu wa 2018/19 hadi 2020/21, hivyo kuiongezea Tanzania pointi na kuwa moja kati ya nchi 12 zenye sifa ya kuingiza idadi hiyo katika mashindano hayo yanayoandaliwa na Shirikisho la Soka barani Afrika, CAF, yaani mbili Kombe la Shirikisho na mbili Ligi ya Mabingwa.

Kwa mantiki hiyo, tukiweka itikadi zetu za klabu mbali, ushindi wa timu yoyote kwenye michuano ya kimataifa si mafanikio tu kwa klabu husika, bali ni kwa Tanzania kwa ujumla, hivyo huu ni wakati sahihi kwa Watanzania wote kuwaunga mkono wawakilishi wetu hao kimataifa.


Tunatambua tayari CAF imepiga maarufu mashabiki kuhudhuria uwanjani kutokana na janga la ugonjwa wa COVID-19, unaokabili duniani kwa sasa, lakini hiyo haiwezi kuwa sababu ya kushindwa kuwapa sapoti wachezaji na timu zetu hizo kimataifa.

Katika hilo, leo tungependa kuona nchi yote ikibadilika rangi na kuwa bluu na machungwa kwa kuvaa jezi za Azam FC huku kesho rangi hizo zikibadilika na kuwa kijani na njano ambazo zinazovaliwa na Yanga.

Kwa kufanya hivyo, kila wanapopita wachezaji na kushuhudia hali hiyo, watatambua kuwa mashabiki na Watanzania kwa ujumla wapo nyuma yao, hivyo wanadeni kubwa la kuwalipa kwa kuhakikisha wanapata matokeo uwanjani.

Hivyo, kubwa kwa sasa tunawatakia kila la kheri wawakilishi wetu hao kimataifa, lakini kuanzia viongozi wa klabu, benchi la ufundi hadi kwa wachezaji, hawana budi kutambua Watanzania wote wapo nyuma yao na wanachokitaka ni matokeo chanya kwa kupata ushindi wa kishindo na si vinginevyo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Barnabas Maro

# Chuki Simba, Yanga ya nini?

**CHUKI** ni hali ya kutokuwapo upendo, hali ya kuwa na roho mbaya, hali ya kuwa na kinyongo. 'Chukia' ni poteza mapenzi, kasirika. 'Chukiza' ni kitendo cha mtu kutopenda mtu mwingine au kitu; kitendo cha kufanya jambo la kuudhi, kitendo cha kiumbe kufika kiwango cha kutopendeza kwa wengine kutokana na matendo yake.

Ndivyo walivyo baadhi ya wanachama na mashabiki wengi wa Simba na Yanga. Mashabiki ni wale wanaofuata upepo kwa timu inayoshinda. Ndio maana leo wapo Simba kwa sababu timu inashinda ila kesho ikifungwa wanahamia Yanga! Hawa hawajui katika mchezo wowote kuna kushinda, suluhu au kushindwa.

Wahenga walituachia methali isemayo: "Chuki humchoma anayeiweka au kuihifadhi. Kwa kawaida chuki humsumbua anayeiweka au kuihifadhi. Twafunzwa umuhimu wa kutoiweka chuki kwani tunajidhuru wenyewe!

Kesho Jumapili, Yanga itakuwa Uwanja wa Benjamin Mkapa jijini Dar es Salaam kupambana na Rivers United kutoka Nigeria kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika. Ni moja ya timu nne za Tanzania zikiwamo Simba na Azam, zote za Dar es Salaam na Biashara United timu pekee kutoka Bara. Kwa hiyo Tanzania ina timu nne kwenye kinyang'anyiro hicho (kitu au jambo linalowaniwa na watu wengi).

Wanachama na mashabiki wa timu zetu tatu zinazoshiriki mchezo huo wanapaswa kuweka kando tofauti na chuki zao ili kuzishangilia timu zetu za nyumbani kwani tofauti na hilo tutaonekana majuha, yaani watu wenye uwezo mdogo wa kufikiri au kuelewa mambo.

Ni lipi lisilo nduguye na mwamu wake? Maana yake ni jambo au tukio lipi ambalo halina linalohusiana nalo au jenzake (ndugu au mwamu?)

Methali hii hutumiwa kumkumbusha mtu kwamba awafanyiapo wenzake mabaya lazima hata naye ataishia kufanyiwa mabaya. Maana yake tuwafanyiayo wenzetu watatufanyia nayo nasi. Pia hutukumbusha kuwa kila jambo lina jingine linalohusiana nalo!

Twazinduliwa (fanya mtu atoke katika hali ya ujinga au kutoelewa jambo) na wahenga kuwa: "Nia njema ni tabibu, nia mbaya huharibu." Maana yake lengo zuri au azimio zuri ni kama dawa ilhali baya ni uharibifu.

Hii ni methali ya kutumiwa kuwakumbusha watu umuhimu wa kuwa na nia njema au kuazimia, (kitendo cha kutia nia ya kufanya jambo; =kusudio, dhamira) kutenda mambo mema ambayo yanaweza kuwafaidi watu.

Kwa upande mwingine, twaambiwa kuwa "Mwenzako akinyolewa, chako kitie maji." Maana yake umwonapo mwenzako ananyolewa unapaswa kutia kichwa chako maji kujitayarisha kwa kuwa utafuata wewe.

Maana yake ni kumpa wosia au ushauri mtu ambaye mwenzake amefikwa na tatizo au shida kwamba anapaswa kujitayarisha au kutahadhari asije akakumbwa na shida hiyo.

Kwa upande mwingine: "Leo kwako kesho kwa mwenzio." Maana yake jambo linalokupata leo liwe la shida au la raha huweza kumpata mwenzio kesho.

Twanasihiwa kutowacheka wenzetu wanaokumbwa na matatizo kwa kuwa yanaweza kutukumba sisi pia. Huweza kutumiwa kumtanabahisha mtu anayejitapa kwa kuwa na hali nzuri kuwa kesho huenda asiwe na hali hiyo na badala yake awe nayo mwenzake aliyemdharau.

Sasa narudi kwa wanachama na mashabiki wa Simba na Yanga. Watu hawa utadhani malimbukeni yaani watu wanaopata vitu au jambo wasilokuwa na mazoea nalo au kupata kwa mara ya kwanza. Timu hizi mbili ndizo zilizotwaa Kombe la Ligi Kuu mara nyingi zaidi zikiongozwa na Yanga kisha Simba. Hata hivyo, mojawapo inaposhinda, watu hawanywi maji yakashuka itakiwavyo!

Hebu niwaambie kuwa: "Hasama ndimi za moto." Maana ya hasama ni uadui uliopo baina ya Simba na Yanga. Twaambiwa uadui au udawa ni kama ndimi za moto ambazo huchoma. Twahimizwa tujiepushe na uadui ambao unaweza kutuletea maangamizo makubwa.

**marobarnabas@yahoo.com**
**0784 334 096**

HABARI KITAIFA

# Mbaroni tuhuma kukutwa na meno ya tembo

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

JESHI la Polisi mkoani Ruvuma linawashikilia watu wawili kwa tuhuma za kukutwa na meno ya tembo.

Watu hao wawili, wakazi wa kijiji cha Kitanda, wilayani Namtumbo, wanatuhumiwa kwa kukutwa na meno ya tembo yenye uzito wa kilo 12.13 ya thamani ya Dola za Marekani 15,000 (zaidi ya Sh. milioni 34.8).

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Ruvuma, Joseph Konyo, alisema tukio hilo lilitokea Septemba 8, mwaka huu, majira ya saa 6:00 usiku katika Kitongoji cha Mitewa na kwamba watu hao (majina yamehifadhiwa) wenye umri wa miaka 22 na 42, walikamatwa wakiwa wamehifadhi nyara hizo nyumbani.

Alisema uchunguzi wa awali ulibaini kuwa watu hao wanajihusisha na ujangili na huwauzia wafanyabiashara mbalimbali kwa siri nyara hizo na kwamba waliwakamata baada ya kuweka mtego na watafikishwa mahakamani hivi karibuni.

Wakati huo huo, watu 13 wamekamatwa kwa tuhuma za kuua ng'ombe sita wenye thamani ya Sh. milioni tatu na kuwajeruhi kwa kuwakata mapanga ng'ombe 13 mali ya Lela Kinasake (39), mfugaji wa Kijiji cha Mabutu wilayani Tunduru.

Kamanda Konyo alisema tukio hilo lilitokea Septemba 7, mwaka huu, majira ya saa 6:00 usiku katika Bonde la Mto Ruvuma, Kijiji cha Chilundundu Kata ya Nalasi Wilaya ya Tunduru.

Alisema siku hiyo ya tukio, mfugaji Kinasake aligundua kuuawa kwa ng'ombe wake sita na kujeruhiwa kwa kukatwa mapanga ng'ombe 13 na kwamba katika tukio hilo watuhumiwa walikuwa na lengo la kuwataka wafugaji watoke katika maeneo ya malisho yaliyoko kandokando ya Mto Ruvuma ambayo kwa kipindi hiki cha kiangazi hutumika kulima mboga.

Kamanda Konyo alisema polisi wanaendelea na uchunguzi na utakapokamilika watuhumiwa watafikishwa mahakamani.




Wanafunzi wa Darasa la Saba Shule ya Msingi ya Misheni ya Bethel, Mabibo Makuburi, jijini Dar es Salaam, wakifurahi baada ya kumaliza mitihani ya taifa ya kumaliza elimu ya msingi iliyomalizika juzi. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Bil. 50 kununua mahindi ya wakulima

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan ameidhinisha Sh. bilioni 50 kwa ajili ya kununua mahindi kutoka kwa wakulima ili kuwanusuru na kudodora kwa bei ya zao hilo.

Hatua hiyo imetokana na hoja binafsi kutoka kwa Mbunge wa Kilolo (CCM), Justine Nyamoga, aliyoitoa juzi bungeni kufuatia kusuasua kwa ununuzi wa mahindi ambayo iliungwa mkono na wabunge.

Waziri Mkuu, Kasssim Majaliwa, aliyasema hayo jana bungeni alipokuwa akiahirisha mkutano wa nne wa Bunge la 12 ambao umeahirishwa hadi Novemba 2, mwaka huu.

Alisema serikali imesikia kilio cha wakulima kupitia wabunge na tayari wamepata Sh. bilioni 50 na ununuzi utaanza Septemba 13.

Alizitaja hatua zingine ambazo serikali imechukua ili kunusuru bei ya zao hilo kuwa awali serikali ilitoa Sh. bilioni 15 kuwezesha Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) kununua mahindi maeneo mbalimbali nchini na Sh. bilioni 10 kwa Bodi ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko (CPB) ili kuongeza mtaji wa ununuzi wa mazao.

"Naiagiza Wizara ya Kilimo izisimamie kwa karibu NFRA na CPB ili zinunue mahindi ya wakulima pekee tena watoke ndani ya nchi. Aidha, ongezeni vituo vya kununulia mahindi hadi wilayani na kwenye miji midogo," alisema.

Waziri Mkuu alisema serikali imetafuta masoko ya mahindi kwa kukamilisha mikataba mipya ya ununuzi wa mahindi Sudan Kusini, Jamhuri ya Kidemokrasi ya Congo (DRC) na Zimbabwe kama njia ya kuhakikisha wakulima wanapata soko la mahindi waliyozalisha.

"Hatua nyingine tuliyochukua ni kufungua mipaka kwa kipindi cha miezi miwili kwa ajili ya masoko ya nje ya nchi ambapo vibali vya usafirishaji hutolewa bure kupitia ofisi za wakuu wa wilaya na kwa njia ya mtandao ili wafanyabiashara kuvipata kwa urahisi. Upelekaji wa chakula utafanywa kwa umakini mkubwa ili kuhakikisha nchi inaendelea kuwa na hifadhi ya kutosha ya chakula," alisisitiza.

Alizitaja hatua nyingine kuwa ni kuwaunganisha wafanyabiashara wa nafaka hapa nchini na wafanyabiashara wa nje kupitia Balozi za Tanzania na kuongeza thamani ya mazao.

Mbali na ununuzi wa nafaka, Waziri Mkuu alisema serikali inafuatilia mwenendo wa upatikanaji wa mbolea ili kuhakikisha bidhaa hiyo inapatikana kwa wingi na bei nafuu.

**IN THE HIGH COURT OF TANZANIA**
**(COMMERCIAL DIVISION)**
**AT DAR ES SALAAM**
**COMMERCIAL CASE NO. 3 OF 2021**
**KNAUF GYPSUM TANZANIA LIMITED……………………….PLAINTIFF**
**VERSUS**
**DIGITAL AUCTION MART ………………………………………DEFENDANT**
**DECREE**

WHEREFORE; The Plaintiff humbly prays for the following reliefs:-

a) Payment of Tshs 280,160,275.74/= being the amount that Defendant failed to remit to the Plaintiff for vehicle and machines purchased and transportation of gypsum stone and coal according to the agreements.
b) Payment of general damages as may be assessed by this Honorable Court.
c) Payment of interest at commercial rate prevailing at the date of judgment, or at such as the Honourable Court may deem fit and just, accruing and computed from the date of judgment of this suit.
d) Four costs of this suit; and
e) Any other relief(s) that this Honorable Court may deem fit and just to grant

This matter coming for Judgment on 20th day of August, 2021 before Hon B. K. Philip, Judge in the presence of Advocate Anwaar Katakwaliba holding brief for Advocate Ester Peter for the Plaintiff and in absence of the Defendant.

**THIS COURT DOTH HEREBY ORDER THAT:**

i. That the Defendant shall pay the Plaintiff a sum of Tshs. 242,900,000/=
ii. That the Defendant shall pay the Plaintiff interests on the decretal sum in item (i) herein above at the Court rate of 7% from the date of judgment to the date of payment full.
iii. The costs of this case shall be borne by the Defendant.

Given under my hand and seal of the court on this 20th day of August, 2021.

THE HIGH COURT OF TANZANIA COMMERCIAL DIVISION

……………………………………
**SUCCESSOR JUDGE**
**31/8/2021**

Extracted on this **31st day of August 2021.**

216453901

# Kesi kukutwa nyaraka za serikali yanguruma

**Na Paulina Chimeledya,** TUDARCO

UPANDE wa ushahidi katika kesi inayowakabili watu watatu wanaodaiwa kukutwa na nyaraka za serikali, umewasilisha vielelezo katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu.

Washtakiwa katika kesi hiyo ni Ashraf Maumba, Mohaud Zuber na Mwamba Seif ambao wote kwa pamoja wanatuhumiwa kukutwa na nyaraka za serikali katika mtaa wa Mgogoso, Buguruni Mnyamani, Ilala jijini Dar es Salaam.

Vielelezo vya nyaraka za ushahidi vilikabidhiwa mahakamni juzi na Mpekuzi Msaidizi Askari Emmanuel Mmari, mbele ya Hakimu Mkazi Joseph Lwambano.

Akitoa ushahidi mahakamani hapo, Mmari alieleza nanna alivyopata taarifa kutoka kwa msiri, aliyemweleza kuwa kuna nyumba inayosadikika kujishughulisha na uhalifu na kwamba baada ya kupata taarifa hiyo, aliwachukua askari wenzake na kwenda katika nyumba hiyo kwa upekuzi.

Mmari alidai kuwa kwenye upekuzi huo, waliambatana na Mjumbe wa Nyumba 10 wa mtaa huo, Zaituni Ally Rajabu, pamoja na mwangalizi wa nyumba hiyo, Ramadhani Birunga.

"Julai 8, 2016 majira ya saa 3:00 tulifika nyumbani hapo na kutoa taarifa kwa uongozi wa serikali za mtaa kwamba tukampata mjumbe wa nyumba 10 na kuongozana naye eneo la nyumba hiyo. Tulijitambulisha na kuanza upekuzi ambao ulifanikisha kukuta vielelezo vya nyaraka mbalimbali za serikali," alidai.

Mmari alitaja baadhi ya nyaraka walizozikuta ni pamoja na mihuri, vyeti vya elimu, leseni, kompyuta nne, ni nyaraka za Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), fomu zenye nembo ya Baraza la Taifa la Mitihani na mihuri.

Kesi hiyo imeahirishwa hadi Septemba 22, mwaka huu. Hakimu Lwambano aliwataka mawakili wa pande zote kuhakikisha mashahidi watakaoshindwa kufika kutoa ushahidi kupata vielelezo vya maelekezo yao juu ya sababu ili kesi isisimame na kutenda haki pande zote mbili.

# Waziri asimamisha uzinduzi uuzaji wa nyumba za NHC

**Na Munir Shemweta,** DODOMA

NAIBU Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, amesitisha uzinduzi wa uuzaji nyumba 300 za mradi wa Iyumbu katika Jiji la Dodoma mpaka Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) litakapokamilisha ujenzi wa mradi huo.

NHC hivi karibuni ilitangaza kuanza uzinduzi rasmi wa uuzaji nyumba 300 kwenye mradi wa Iyumbu Septemba 14, mwaka huu.

Akizungumza katika ziara ya kushtukiza kwenye mradi huo jana, Dk. Mabula, alisema lengo la Wizara ya Ardhi ni kuwa mradi wa nyumba hizo ukamilike ndipo zianze kuuzwa kwa wale wanaozihitaji. ''Makubaliano ya kazi za ujenzi wa nyumba zinakwisha kwanza na mtu anapewa funguo na hati yake. Lakini leo utapomuuzia mtu nyumba ambayo haijakamilika unamuuzia nini? Au unamuuzia nyumba 'in progress'? Lengo letu ni kumuuzia nyumba iliyokamilika," alisema Dk. Mabula.

Naibu Waziri aliongeza kuwa wananchi wanaohitaji kununua nyumba hizo wanaweza kuonyesha nia kwa kufika ofisi za NHC ili kuelezwa taratibu na hatua za kufanya kabla ya uuzaji kuanza.

Mkurugenzi wa Ujenzi wa NHC, Mhandisi Haikamen Mlekio, alisema shirika lake kwa sasa liko hatua za mwisho za ukamilishaji mradi wa nyumba hizo na kuongeza kuwa watahakikisha mradi unakamilika kwa wakati kwa kufanya kazi usiku na mchana.

Aidha, Naibu Waziri alilitaka shirika kuongeza kasi katika ujenzi wa mradi huo wa Iyumbu na kusisitiza kuwa lazima uwe katika viwango vinavyotakiwa kwa kuzingatia sheria na taratibu za kimazingira.

"Ninyi ni waendelezaji kiongozi na wanaokuja wote waelewe kiwango cha kazi za NHC na viwango vyenu viwe vimekidhi mahitaji na kuzingatia sheria na taratibu zikiwamo za kimazingira ili wengine wajifunze. Lazima kila kinachofanyika kiende katika utaratibu na wizara ijivunie kuwa na shirika," alisema Dk. Mabula.



Naibu Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angeline Mabula, akikagua sehemu ya vifaa vitakavyotumika kukamilisha nyumba za mradi wa nyumba 300 za Iyumbu jijini Dodoma, alipokwenda kukagua maendeleo ya mradi huo jana. **PICHA: MUNIR SHEMWETA**

# Wapewa elimu usalama, ubora muhogo

**Na Mwandishi Wetu,** KILINDI

WAKULIMA na watumiaji wa bidhaa za muhogo katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilindi na maeneo yanayozalisha zao hilo kwa wingi, wamepatiwa elimu kuhusu usalama na ubora.

Elimu hiyo ilitolewa kwa wakulima na watumiaji wa zao hilo na maofisa wa Shirika la Viwango Tanzania (TBS) waliotembelea wakulima na watumiaji wilayani hapa mkoani Tanga kwa lengo la kuwapa elimu hiyo.

Akizungumza wakati wa mafunzo hayo, Ofisa Udhibiti Ubora wa TBS, Ashura Kilewela, alisema pamoja na mambo mengine, wakulima na watumiaji wa bidhaa za muhogo walielimishwa kuhusu uwapo wa sumu asili katika zao hilo pamoja na umuhimu wa zao kwa chakula.

Licha ya umuhimu wa zao hilo kwa chakula, alisema huathiriwa na kemikali ya sumu asili na aliwaambia washiriki wa mafunzo hayo kuwa sumu asili katika muhogo hutokana na uwepo wa kemikali inayozalishwa na mmea wenyewe inaoitwa 'sianidi'.

Kwa mujibu wa Kilewela, kiasi cha kemikali ya 'sianidi' katika muhogo hutofautiana kutegemea aina ya muhogo husika na ladha yake.

Alitoa mfano akisema muhogo mtamu una ladha tamu na kiasi kidogo cha kemikali ya 'sianidi', wakati muhogo mchungu una ladha chungu na kiasi kikubwa cha kemikali ya sianidi.

Alitaja sababu zinazochangia kuongezeka kwa kiasi cha sumu asili katika muhogo kuwa ni aina ya muhogo uliolimwa ambapo muhogo wa aina mbalimbali huzalisha kiasi tofauti cha kemikali ya 'sianidi'.

Pili, alisema ni hali ya hewa kwamba kiasi cha sianidi katika muhogo huongezeka zaidi wakati wa ukame na tatu kuwa ni aina ya udongo unapolimwa.

Kwa mujibu wa Kilewela, kiasi cha kemikali ya 'sianidi' katika muhogo hutofautiana kati ya eneo moja na lingine kutegemea aina ya udongo wa eneo la kilimo hata kama mbegu iliyotumika ni ya aina moja.

Sababu ya nne ni muda wa uvunaji muhogo ukichelewa kuvunwa, huchangia kuongeza kiasi cha kemikali ya sianidi kutegemeana na aina ya muhogo uliopandwa. Kilewela alisema kwa wastani muhogo huchukua miezi minane hadi 12 hadi muda wa kuvuna na mingine hadi miezi 24.

Aliwataka washiriki wa mafunzo hayo kufahamu kuwa aina ya udongo huchangia kuongezeka au kupungua kwa sianidi katika muhogo.

Ofisa Usalama wa Chakula Mkuu wa TBS, Dk. Candida Shirima, alisema mlaji anaweza kupata madhara ya kiafya yatokanayo na sumu asili aina ya sianidi endapo atakula chakula kitokanacho na muhogo chenye kiasi kikubwa cha kemikali hiyo.

"Chakula hicho kinaweza kuwa muhogo uliomenywa na kuliwa mbichi, kupikwa, bidhaa zitokanazo na muhogo au majani yake (kisamvu)," alisema alisema Dk. Shirima.

Alisema 'sianidi' hujitokeza baada ya muda mfupi au mrefu kutegemea kiasi cha kemikali hiyo kwenye chakula kilicholiwa, umri na hali ya afya ya mlaji.



# Miji 28 kunufaika na miradi ya maji

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imesema hivi karibuni itaanza kutekeleza miradi ya maji katika miji 28 ambapo zaidi ya Sh. trilioni moja zimepatikana kutoka Benki ya Exim.

Waziri wa Maji, Jumaa Aweso, aliyasema juzi jijini hapa alipokuwa akizungumza na wahariri na wawakilishi wa vyombo mbalimbali vya habari vya Dodoma.

Alisema katika mkakati wa kuhakikisha wanafikia asilimia 95 ya upatikanaji wa maji mjini, serikali imepata fedha hizo kutoka serikali ya India kupitia benki hiyo kutokana na uhusiano mzuri uliopo.

"Tulikuwa tumepata fedha zaidi ya Dola za Marekani milioni 500 ambazo zinatokana na uhusiano mzuri wa Rais na Serikali ya India kupitia Exim Bank sawa na zaidi ya Sh. trilioni moja kwa miji 28.

"Huu mradi ulikuwa wa muda mrefu sana changamoto yake kubwa ilikuwa suala la utoaji wa kibali kwa hiyo tulifanya mazungumzo kupitia Wizara ya Fedha na watu wa Exim, kibali tumeshakipata niwaeleze Watanzania miradi ile ya miji 28 inaenda kuanza hivi karibuni," alisema.

Alibainisha kuwa tayari kibali kimepatikana na makandarasi wameshajulikana na kwa sasa wapo kwenye hatua ya kukubaliana na baada ya hapo watasaini mikataba ya utekelezaji wake ili Watanzania wapate majisafi na salama.

Waziri Aweso aliitaja miongoni mwa miji itakayonufaika na mradi huo kuwa ni Makambako, Wanging'ombe, Muheza na Handeni.

Kuhusu mita za luku za maji, Aweso alisema serikali itaanza kuwa na luku za maji ili kuondokana na tatizo la malalamiko ya ankara za maji ambapo tayari wameanza kupata watu wenye teknolojia mbalimbali.

"Tutazingatia ubora pamoja na kufungua milango hiyo na gharama ili isifungwe kwa gharama kubwa na kuwasaidia wananchi, na hili jambo litafanyika kwa haraka ili kuondokana na kero za ubambikizaji bili," alisema.

# Bunge laridhia kuanzishwa eneo huru la biashara Afrika

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

BUNGE limeridhia mkataba wa uanzishwaji wa eneo huru la biashara la Afrika (AfCFTA) ili kuongeza kiwango cha ufanyaji biashara miongoni mwa nchi za Afrika.

Akitoa maelezo kuhusu azimio la kuomba Bunge kuridhia mkataba huo Bungeni jana, Waziri wa Viwanda na Biashara, Prof. Kitila Mkumbo, alisema mwaka 2013, Wakuu wa Nchi na Serikali wa Umoja wa Afrika walikubaliana kutengeneza Dira ya Afrika ya miaka 50 ijayo.

Alisema dira hiyo ililenga kuchochea na kuharakisha mabadiliko makubwa ya kisiasa, kijamii, kiuchumi na kiteknolojia kwa Afrika na moja ya miradi ya kielelezo ni kuanzishwa kwa AfCFTA.

Prof. Mkumbo alisema lengo ni kuchochea na kuharakisha ukuaji wa kiwango cha biashara ndani ya Afrika na kutumia biashara kama injini ya kukuza maendeleo ya uchumi katika bara hilo.

"Matarajio ya hatua hiyo ni kuona kuwa kiwango cha ufanyaji biashara miongoni mwa nchi za Afrika kikiongezeka kutoka asilimia 17 ya sasa hadi asilimia 22 ifikapo mwaka 2025 na kufikia asilimia 40 ifikapo mwaka 2040," alisema.

Pia alisema kwa sasa kiwango cha kufanya biashara ndani ya Bara la Afrika ni kidogo

kulinganisha na mabara mengine, kwa mfano Ulaya asilimia 68.1, Asia (59.4) na Amerika (55).

Waziri huyo alibainisha kuwa maeneo muhimu na malengo ya mkataba wa AfCFTA linahusisha nchi 55 wanachama wa Umoja wa Afrika ambazo kwa sasa zina zaidi ya watu bilioni 1.2 na pato la taifa la jumla ya Dola za Kimarekani trilioni 3.4.

"Mkataba wa AfCFTA una sehemu kuu saba ambazo ni itifaki ya biashara ya bidhaa, itifaki ya biashara ya huduma, itifaki ya usuluhishi wa migogoro, itifaki ya uwekezaji, itifaki ya haki miliki ubunifu, itifaki ya sera ya ushindani na itifaki ya biashara mtandao," alisema.

Alitaja matokeo chanja ya kuridhia mkataba huo ni kupatikana kwa masoko mapya ya mazao ya kilimo na kuimarika kwa mnyororo wa thamani wa mazao yanayohusisha wakulima wadogo kama vile alizeti, pamba, karafuu, viungo, matunda na mbogamboga kutokana na kuongezeka kwa soko la bidhaa ambazo zitazalishwa nchini.

Akitoa maoni ya Kamati ya Bunge ya Viwanda, Biashara na Mazingira, Mwenyekiti wa Kamati hiyo, David Kihenzile, alishauri mambo saba kuhusu mkataba huo ikiwamo serikali ifanye tathmini ya utekelezaji wa mikataba ya aina hiyo ambayo Tanzania imeingia kama vile EAC na SADC ili kubaini kero zilizojitokeza wakati wa utekelezaji wake na kujipanga vyema kabla ya kuanza mkataba huo.



Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu, akizungumza na watumishi wa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) katika mkutano wa kwanza wa Baraza la Wafanyakazi wa tume hiyo, jijini Dodoma juzi. **PICHA: RENATHA MSUNGU**

# Waziri ataka taarifa uhaba walimu

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu, ametoa wiki mbili kwa halmashauri zote nchini kuwasilisha taarifa kuhusu uhaba wa walimu wa shule za msingi na sekondari kwenye maeneo yao.

Aidha, ameiagiza Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) kuanzisha mfumo wa teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) wa kuwatambua walimu wanaojitolea kazini ili ajira zinapotolewa wapewe kipaumbele.

Akifungua mkutano wa Baraza la Wafanyakazi wa TSC juzi, Waziri Ummy, alisema taarifa hiyo itasaidia kutatua uhaba wa walimu mara ajira zinapotolewa.

Ummy alisema hadi Septemba 21, mwaka huu, takwimu za uhaba wa walimu ziwe zimewasilishwa ofisi kwake ili serikali ijue wapi inatakiwa kutoa ajira ili kuziba mapengo.

Kuhusu mfumo, waziri huyo alisema utasaidia kujua walimu wote wanaojitolea katika shule mbalimbali hapa nchini na masomo wanayofundisha ili kuwasaidia kupata ajira kwa haraka zinapotangazwa na serikali.

"Ninaomba mfanye hilo suala la kutengeneza mfumo huo, kwa sababu ajira zikitoka unakuta malalamiko ni mengi, lakini mnakuwa hamna uhakika wa nani amejitolea kazini na mwisho wa siku anapata ajira ambaye hajawahi hata kujitolea," alisema Ummy.

Alitaka baraza hilo kujadili suala hilo na kuliwekea mikakati huku akisema kitendo cha kuwapa ajira walimu hao wa kujitolea kitafanya wengi wakae kwenye maeneo yao wanayopangiwa hasa maeneo ya pembezoni.

Awali, Katibu Mtendaji wa TSC, Paulina Mkwama, aliishukuru serikali kwa kuwapandisha walimu vyeo, kulipa malimbikizo ya madeni hatua ambayo imesaidia kupunguza malalamiko ya walimu.



# Muswada Ofisi ya Mufti wapitishwa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAJUMBE wa Baraza la Wawakilishi wamepitisha muswada wa kuanzishwa kwa Ofisi ya Mufti wa Zanzibar ambao sasa utaiwezesha Zanzibar kujiunga na taasisi za maendeleo ya Kiislamu.

Mwanasheria Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Dk. Mwinyi Talib Ali, alisema muswada huo lengo lake kuipa uwezo Ofisi ya Mufti katika utekelezaji wa majukumu yake ya kusimamia mambo yote ya Kiislamu kwa upande wa Zanzibar.

Akizungumza jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi, Chukwani, nje ya mji wa Zanzibar, alisema kuanzishwa kwa Ofisi ya Mufti sasa kutaiwezesha kuwa na uhusiano na ushirikiano na taasisi mbalimbali za maendeleo ya kiislamu zenye maslahi ya ofisi na taifa kwa ujumla.

Mapema, akijibu hoja za wajumbe waliochangia muswada huo, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala wa Bora, Haroun Ali Suleiman, alisema muswada huo lengo lake ni kuweka sawa mambo yote yanayowahusu Waislamu na utaratibu wake.

Alisema Ofisi ya Mufti ndiyo yenye uwezo wa mwisho wa kushughulikia mambo yote ya kuandama kwa mwezi na kuondoa hitilafu na mivutano.

Haroun alisema mivutano ya kuandama kwa mwezi ni changamoto kubwa ambayo husababisha mivutano miongoni mwa jamii ya Waislamu nchini na sasa ufumbuzi wake umepatikana.

"Changamoto kubwa iliyokuwa ikiwakabili Waislamu ni suala la kuandama kwa mwezi kwa nyakati tofauti ikiwamo kabla ya kuingia kwa Ramadhani na nyakati za sikukuu za Kiislamu. Mambo yote hayo sasa yatasimamiwa na Ofisi ya Mufti wa Zanzibar," alisema.



Mwenyekiti wa Chama cha ADA-Tadea ambaye ni Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi nafasi maalum za Rais, Juma Ali Khatib, akipata chanjo ya corona kutoka kwa mtaalamu wa afya, zoezi linaloendelea katika baraza hilo, Chukwani Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

## TADEA yamuunga mkono Jaji Mutungi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MWENYEKITI wa Chama cha ADA -TADEA, Juma Ali Khatib, amesema anaunga mkono kauli ya Msajili wa Vyama vya Siasa ya kuvitaka vyama vya siasa kukaa na Jeshi la Polisi na kufanya mazungumzo ili kufikia makubaliano.

Akizungumza jana na waandishi wa habari katika ukumbi wa Sanaa Rahaleo, mjini Unguja, alisema anaunga mkono kauli ya Jaji Francis Mutungi ya kukaa pamoja na Jeshi la Polisi na kufanya mazungumzo ya kuafikiana kuhusu ufanyaji wa mikutano kwa wanasiasa.

Alisema kwa miaka mingi vyama vya siasa vimekosa nafasi ya kufanya mikutano ya hadhara, hivyo ana imani kuwa mkutano huo wa pamoja utakuwa mwarobani wa kufanya mikutano ya hadhara.

Juma alisema Tanzania ina amani na utulivu, hivyo si vyema kusababisha mivutano na Jeshi la Polisi, jambo ambalo halikubaliki kuona linatokea.

Alisema Msajili wa Vyama vya Siasa amekuwa na moyo safi na thabiti wa kuwaeleza viongozi wa vyama vya siasa kuwa wakae meza moja na polisi ili kupitisha uamuzi sahihi na kuepukana na mivutano kati yao juu ya kuzuiwa kufanya mikutano.

"Jaji Francis Mutungi maneno aliyoyasema kuwaambia viongozi wa vyama vya siasa ni mazuri kabisa kwani yanajenga umoja. Sasa anapotokea kiongozi akalipinga neno hilo na kutaka kuleta uvunjifu wa amani, sisi TADEA hatukubaliani naye," alisema.

Njia nzuri ya kupata mustakabali mzuri kati yao na serikali, alisema ni kukubali kukaa na jeshi hilo ili kuzungumza kwa pamoja kwa lengo la kufikia makubaliano.

Mwenyekikti huyo aliwaasa wananchi wa vyama vya siasa kuachana na baadhi ya watu wanaotaka kuleta migogoro katika nchi na kuwataka kudumisha amani iliyopo.

Katika hatua nyingine, mwenyekiti huyo ambaye ni Mjumbe wa Baraza la Wawakilishi kwa nafasi maalum za kuteuliwa na Rais, jana aliungana na baadhi ya wajumbe wa baraza hilo kupata chanjo ya corona inayoendelea kutolewa katika Baraza la Wawakilishi.

Akizungumza baada ya kupata chanjo hiyo, Juma alisema chanjo ya kujikinga na ugonjwa hatari wa corona ni muhimu kwa ajili ya kujulinda na maambukizi ya virusi hivyo.

# SMZ yaendelea kutafiti hifadhi ya ardhi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Uvuvi na Uchumi wa Bluu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Abdalla Hussein Kombo, amesema serikali inaendelea na utafiti kwa kushirikiana na wafadhili kuhusu mpango endelevu wa hifadhi ya ardhi na matumizi sahihi hatua ambayo itasaidia kudhibiti uvuvi haramu.

Hayo aliyasema jana katika kikao cha Baraza la Wawakilishi wakati akijibu swali la Mwakilishi wa Kwahani, Yahya Rashid Abdalla, aliyetaka kujua mikakati inayochukuliwa ya kulinda rasilimali za baharini.

Waziri Kombo alisema suala la uhifadhi na mipango endelevu ya matumizi ya bahari limepewa kipaumbele katika mikakati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuelekea uchumi wa bluu.

Alisema uchumi wa bluu unahitaji udhibiti muhimu kwa kutunga sera nzuri zitakazohakikisha zinawalinda wananchi pamoja na wawekezaji watakaowekeza katika sekta hiyo.

Kombo alisema tayari maeneo ya ukanda wa hifadhi ya uvuvi katika kisiwa cha Pemba PECCA utafiti umefanywa na kuonyesha kuwapo kwa hazina kubwa ya samaki na rasilimali zingine.

Alisema hatua hiyo imeifanya serikali kulitangaza eneo hilo kuwa maalumu kwa uhifadhi wa mazingira ya baharini ambayo inapiga marufuku uvuvi haramu katika maeneo hayo.

"Eneo la Ukanda wa Hifadhi wa Mkondo wa Pemba (PECCA) limetangazwa rasmi katika gazeti la serikali na kutambuliwa ambapo uvuvi haramu umedhibitiwa na rasilimali ya samaki ikilindwa," alisema.

Aidha, alilitaja eneo la kisiwa cha Mnemba kuwa tayari limefanyiwa utafiti na kuingizwa katika mpango wa hifadhi ya uvuvi wa baharini huku yakiwapo mafanikio makubwa.

"Mheshimiwa Spika napenda kuwajulisha wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba kuwapo kwa maeneo ya hifadhi ya baharini kwa kiasi kikubwa yamesaidia kulinda rasilimali na kudhibiti uvuvi wa haramu katika maeneo hayo," alisema.



**WENGI WAMWONEA HURUMA BRITNEY SPEARS** Uk.14







**KUMBE KWELI**

# Vanessa ashindwa kuukana uongo

SIKU kadhaa zilizopita, mwanamuziki wa Bongo Fleva, Vanessa Mdee, alikuja juu akiwalaumu watu kuzua uongo kwamba eti yeye ni mjamzito, kitu ambacho si cha kweli.

Msanii huyo ambaye kwa sasa anaishi Marekani na mpenzi wake raia wa Nigeria, Rotimi, alidiriki kusema kwamba uvumi huo unamfanya mama yake kupata presha na kuomba wamuache mzee wa watu.

Hata hivyo, haikupita miezi mitatu Vanessa, amethibitisha kwamba ni mjamzito huku akionekana tumbo kubwa na ikiashiria wakati akikana tayari alikuwa mjamzito wa mizei kadhaa.

Mpenzi wake Rotimi, aliweka picha katika ukurasa wake wa Instagram, akisema wanatarajia kupata mtoto wa kiume siku za hivi karibuni.

Wachambuzi wanaofuatilia maisha ya mastaa, wamesema Vanessa hakujiandaa vizuri kuficha hali yake ili baadaye aweze kuwashtua mashabiki wake, kwani aliacha upenyo na kusababisha watu kujua mapema.

"Vanessa aliacha nafasi watu kujua mapema ujauzito wake, hata alipoamua kusema ukweli halikuwa jambo jipya tena ni muhimu akafahamu namna ya kuficha habari zake," amesema Jackson Nadi.

Hata hivyo, mastaa mbalimbali wamejitokeza kumpongeza na kumtakia afya njema wakati akisubiri kumpokea mtoto wake wa kwanza.

Jux Juma ambaye alikuwa mpenzi wake, alimtakia maisha mazuri na kumwambia ayasahau maisha ya zamani kwani yamepita na sasa waangalie dunia nyingine.

BASI SAWA

## Sikia ya Full Tank ucheke

MSANII Full Tank, ametoa kali ya mwaka kwa kusema anaogopa kifo cha mapema, kwa sababu ataacha vitu vizuri kama chips mayai na kuku.

Akizungumza na eNewz , Full Tank amesema dua zake zote ni kumuomba Mungu ampe maisha marefu, ili aendelee kufaidi Dunia.

"Mimi suala la kufa mapema siliwazi kwa sababu nawazia vitu vingi sana, mfano unakufa mtu unaacha vitu vizuri kama misosi chipsi mayai au kuku" amesema.




## Kala omba yasikukute, utasaga meno

RAPA Kala Jeremiah, amesema huwa anachukia kuona watu wenye fedha wanawaumiza wenzao wa chini kwa kuharibu uhusiano wao wa kimapenzi.

Amesema wazee wenye nazo wanapokonya wake na wapenzi wa watu, na hivyo kusababisha maumivu, vilio na hata kuchanganyikiwa.

"Watu wenye pesa wanapokonya wake na wapenzi wa watu na hicho ni kitu kibaya na imekuwa kilio na maumivu mengi" amesema.






## Ukweli wa Nadia Ntuli anayemliza Drake

HUU ndiyo ukweli wa maisha ya mwanamitindo, Nadia Ntuli, Mtanzania pekee aliyeimbwa katika wimbo unaopatikana katika Albam mpya ya mwanamuziki maarufu Drake.

Nadia ameibua majadala mkali katika mitandao ya kijamii baada ya vyombo vikubwa duniani, kumzungimzia binti huyo, ambaye inaaminika alikuwa rafiki wa mwanamuziki huyo kwa muda mrefu.

Hata hivyo, Nadia alifariki dunia mwezi januari mwaka huu akiwa Dubai, baada ya kumaliza likizo yake ya mapumziko nchini Tanzania.

Mama yake mkubwa aliyejitambulisha kwa jina la Bupe, amesema kitendo cha msanii huyo mkubwa kumkumbuka binti yao ni jambo kubwa na lenye kufurahisha.

"Tulivyosikia wimbo tumefurahi kuona mtoto wetu ameweka kumbukumbu nzuri kwa mtu maarufu na hata kumtaja katika wimbo wake.

Nadia amezaliwa na mama Mtanzania na baba yake Muingereza, lakini maisha ya wazazi wake wote yapo hapa nchini.



## Selina Ephraim atamba 'Ni Wakati Wake'

BAADA ya kimya cha muda mrefu mwimbaji anayekuja kwa kasi kwenye muziki wa Injili nchini, Selina Ephraim, amewaomba wapenzi wa muziki huo kuupokea wimbo wake unaoitwa 'Ni Wakati Wake'.

Akizungumza na BT, Selina amesema wimbo huo umegusa maisha yake binafsi na umebeba ushuhuda wake.

"Mimi nimeugua sana, nimepitia vita kubwa ya magonjwa, lakini sijawahi kukata tamaa maana naamini Mungu yupo upande wangu, sio mtu unaumwa ugonjwa fulani basi umeshapaniki unakuwa na hofu kubwa bila kujua hofu ni ugonjwa mkubwa sana kuliko magonjwa mengine tunapaswa kuwa jasiri kwenye nyakati ngumu.

Ameongeza "Siku moja kuna familia ilipatwa na magumu ikawa inalaumu kutokana na ilivyoumizwa, lakini mimi nikawasihi kwamba wanapaswa kumshukuru Mungu na kuamini kuwa ni mapenzi yake,"

Aidha amesema video ya wimbo imeongozwa ba David Mboya wa Scarlet Media na inapatikana katika mtandao wa YouTube.

## Kuachwa sikia hivyohivyo

**Na Adam Fungamwango**

KWA hali ya kawaida ya binadamu, kuachwa na mpenzi ni jambo baya sana, ambalo hataki limtokee.

Mtu anapokuwa na mpenzi na wanapendana, anaona kama dunia yote ni ya kwake. Anatamani aote mabawa aruke juu na kuiambia dunia nzima jinsi gani anapendwa.

Hali inakuwa tofauti sana pale wanapoachana. Na hata mmoja anapoachwa. Unaweza kuomba ardhi ipasuke, ili uingie.

Mtu anayeachwa anaweza kuona kama dunia yote inamuonea. Ataomboleza na kuongea yote.

Wanamuziki na wasanii wanalijua hili. Ni watu anaoishi kwenye jamii na ama yamewakuta au wameyaona. Leo tuna nyimbo zinazowahusu watu walioachwa na wapenzi wao

**KUACHWA-KHALID CHOKORAA**

Wimbo huu ulitoka katikati ya miaka ya 2000, utunzi wake Khalid Chokoraa. Unazungumzia jinsi mtu aliyeachwa anavyojisikia vibaya.

Mbaya zaidi ni kumuona mpenzi wake aliyeamuacha ananenepa, halafu yeye anakonda kwa mawazo. Ni moja kati ya vitu vibaya na usiombe yakukute.

**MAMA RHODA-JOSE CHAMELEONE**

Mwanzoni mwa miaka ya 2000, msanii kutoka Uganda, Jose Chameleone, alitoka na wimbo unaosema 'Mama Rhoda'.

Mtunzi anamlalamikia mama Rhoda kwa nini amemuacha na anamwambia kuwa ipo siku atamkumbuka. Ni kwamba mama Rhoda amemkimbia na kumuachia watoto.

**SHAHADA YA UVUMILIVU-DDC MLIMANI PARK**

Ni wimbo wa masikitiko sana. Ulitungwa mwishoni mwa miaka ya 1980. Ni stori ya mtu anayetunukiwa shahada ya uvumilivu na rafiki zake. Ni baada ya kukimbiwa na mkewe, ambaye alirubuniwa na mwanaume kwa ahadi ya pesa na kujengewa nyumba. Jamaa ilimuuma sana, lakini hakulipiza kisasi cha hasidi aliyemrubuni mkewe. Badala yake aliacha kama ilivyo, lakini akiugulia maumivu moyoni.

**TUMA-JUWATA JAZZ BAND**

Katikati ya miaka ya 1980, Tx Moshi William alitunga wimbo wa 'Tuma', unaomzungumzia mtu aliyesimama kwenye kona ya barabara za Uhuru na Msimbazi akiatazama wanaokwenda na kurudi kama anaweza kumuona mpenzi wake Tuma, walioahidiana kupelekana kwa wazazi.

Jua liliwaka, hadi lilizama, demu hakuonekana. Jamaa alikuwa amechwa kwenye mataa. Kwa huzuni, jamaa anaombolewa kuwa ni matatizo kumpenda mwanamke mrembo anayependwa na wengi, unaweza kunywa sumu au kujinyonga. Hata hivyo kwa kuwa yeye ni kijana, basi atasonga mbele na maisha mengine.

**MCHUMBA HANITAKI-SIMBA WANYIKA**

Ilikuwa ni mwishoni mwa miaka ya 1970, Willson Peter alipotunga wimbo wa 'Mchumba Hanitaki.'

Jamaa analalamika kuwa mchumba wake, awali alikuwa anampenda na walipanga kuoana, lakini kwa sababu sasa pesa na kazi hana, ameamua kumsaliti na kumkataa mchana kweupe.

Jamaa analalamika alie na nani.





## Hukumu ya Penzi; una dada, unakataaje shemeji?

**Na Adam Fungamwango**

HUKUMU ya penzi ni moja kati ya filamu za kibongo zenye mafundisho mengi kwenye jamii.

Kwanza inafundisha juu ya watoto wa watawala kuheshimu wananchi, kwa sababu utawala wa baba zao siyo wao.

Kuna baadhi ya watoto wa viongozi, wanajiona wao wako juu ya sheria kwa sababu tu ya vyeo vya baba zao. Hii inawafanya wananchi wanyanyasike na kuwaondolea utu wao, huku wakidhalilishwa na kuadhibiwa.

Kuna mafunzo mengine tunayapata kuwa siku zote mwenye dada hakosi shemeji. Ukiwa na dada unatakiwa uheshimu hisia zake. Yeyote ambaye dada yako atampenda, basi ni shemeji yako. Ni kama wewe utakapompenda msichana yeyote. Kaka yake akifanya roho mbaya, ni lazima utasononeka kuona hufanyiwi haki.

Hivyo hivyo hata kwa wanawake. Anayempenda kaka yako, huyo ni wifi yako. Na wala huwezi kumlazimisha kaka yako kumpenda msichana unayempenda wewe, hata awe shoga yako mkubwa.

Imechezwa na wasanii Fadhili Msisiri, Debora Dickson, Evance Lusunzu, Luiza Jafeth, Mzee Jengua na wengine wengi.

Himaya fulani inamilikiwa na mfalme Simba. Huyu alikuwa na watoto wawili. Wa kike na wa kiume. Binti mfalme alikuwa mkarimu na asiyeringia cheo cha baba yake. Mtoto wa kiume wa mfalme, yeye akawa kama mfalme mwenyewe. Ni tishio kwa wananchi wote wa himaya hiyo. Akaogopeka kwa kufanya matendo ya kikatili na mauaji, wakati mwingine, bila baba yake kufahamu.

Anambaka msichana mmoja anaitwa Michi na kumuua. Kwa bahati mbaya kijana Miki anaona tukio hilo. Naye anauawa kwa madai ya kumuua msichana Michi aliyeuawa na mtoto wa mfalme.

Kijana mmoja kutoka mjini Barton anaingia kwenye himaya hiyo kumsalimia mama yake mzazi. Anatokea kupendana na binti mfalme. Hii inamkera sana kijana wa mfalme na kuazimia kumuua.

Siku moja anawafuma laivu. Anachukua mkuki, kwa ajili ya kumuua Barton. Mita chache kabla haujafika tumboni, binti mfalme anakatiza mbele kumkinga mpenzi wake, unamuingia yeye tumboni.

Kijana mfalme sasa akamsingizia Barton kuwa ndiye aliyemuua dada yake. Mfalme Simba anaamuru Barton azikwe akiwa hai. Vyovyote alivyofikiri kama yuko sawa, alikosea. Mzimu wa Batron sasa unakuwa unawatesa kwenye himaya hiyo. Anawatokea wabaya wake wote na kuanza kuwaua mmoja baada ya mwingine.

# Card B, Offset wapata mtoto wa pili



RAPA wa Marekani Cardi B, na mume wake Offset, wamepata mtoto wao wa pili.

Mwanamuziki huyo mwenye vituko vingi, amethibitisha kupitia akaunti yake ya Instagram, baada ya kuweka picha ikiwa na sura yake, mume wake na mtoto huyo.

Offset, pia aliweka katika ukurasa wake wa Instagram, picha yake, ambayo inamuonyesha akimbeba mtoto mchanga.



## Wamwonea huruma Britney Spears

MASHABIKI wa mwanamuziki Britney Spears, sasa wanasubiri kuona kitakachotokea baada ya baba mzazi wa msanii huyo, kuwasilisha ombi la kujitoa usimamizi wa kazi za mwanawe.

Wiki hii Jamie Spears, aliwasilisha ombi hilo katika mahamaka ya Los Angeles, akitaka kusitisha hadhi yake kama mtunzaji na msimamizi wa mali za binti yake aliyokuwa nayo kwa kipindi cha miaka 13.

Mara kadhaa, Britney amekuwa akijaribu muondoa baba yake kwenye jukumu hilo akidai kunyanyaswa na kufanywa kama mtumwa.

## OCJ azindua EP yake kiaina

MWANAMUZIKI wa Nigeria, OCJ ameachia EP yake mpya yenye nyimbo tisa.

OCJ ameungana na mastaa kadhaa nchini humo waliozindua EP au Album mpya mwaka huu, ambapo ameipa jina la “The African Prince” kama kuonyesha thamani ya kazi yake.

Moja ya wimbo mkali inayopatikana katika EP yake ni “Familiar ‘ ambao umepata umaarufu ndani na nje ya nchi hiyo.





## Michael Williams aaga dunia

MSANII mkongwe wa filamu wa Marekani, Michael K. Williams, amefariki dunia.

Williams amekutwa amefariki siku ya jumatatu ndani ya nyumba yake iliyopo Brooklyn.

Imeelezwa chanzo cha kifo hicho kinatokana na kuzidisha kiwango cha dawa za kulevya, kutokana na mwili wake kukutwa ukiwa na dawa aina ya paraphernalia, ambayo ilikuwa pembeni yake.

Mwigizaji huyo anajulikana kutokana na kazi zake nzuri kama tamthilia ya Omar Little’ “The Wire” Chalky White na “Boardwalk Empire.”

## Kylie Jenner apata ujauzito

MWANAMITINDO na mshiriki wa shoo ya maisha halisi wa televisheni, Kylie Jenner, imefahamika anatarajia kupata mtoto wa pili.

Staa huyo kupitia ukurasa wake wa Instagram, ameweka picha akionekana katika hali hiyo ya ujauzito na inaelezwa mtoto huyo wa pili ni wa Travis Sccot, ambaye alitengana naye.

Katika video hiyo inaonyesha kipimo cha Janner, kikionyesha alama ya chanya, ambayo inathibitisha ni mjamzito.



MAKALA

# Kinamama katika uandishi habari bila rushwa ngono inawezekana?

**Na Mary Geofrey**

LICHA ya kwamba tasnia ya habari ikiwa maarufu, lakini nayo inatajwa haiko salama sana katika misukosuko ya unyanyasaji kijinsia kazini.

Inatajwa imo katika orodha ya tasnia, kinamama wanakabiliwa na magumu ya unyanyasaji kupitia rushwa ya ngono. Je, kuna ukweli wa hakika katika hoja hiyo? Nipashe ikiwa sehemu ya mdau, iliamua kuchukua jukumu la kihabari kupata undani.

Sura mojawapo iliyojitokeza katika majumuishi ya makala hii, ni kukosekana hali ya kujiamini pasipo kutetereka kwa baadhi ya kinamama hao, pale vikwazo vinavyojitokeza mbele yao kikazi.

Hofu ya kushindwa 'kufunguka' nafasi ya haki zao pia ushuhuda wake ulijitokeza wazi kwa Nipashe, wakiwamo wanahabari kinamama wazoefu wenye weledi, lakini baadhi yao waligundulika wazito kujitetea.

Kimsingi, suala la haki za dhamana za kitaaluma na wajibu katika eneo la kazi za ki-uanahabari, kinga zake zinajisheheni na kutetewa na sheria za ndani ya nchi.

Pia kitaifa na kimataifa haki zinasimamiwa na sheria za haki za binadamu, vivyo hivyo zinazizohusu ajira, kama Sheria ya Ajira na Uhusiano Kazini, iliyopitishwa mwaka 2004.



Wanahabari wa kike wakitoa zawadi kwa wagonjwa katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH).
**PICHA ZOTE : MTANDAO.**

### UTAFITI WA TAMWA

Chama cha Wanahabari Wanawake (TAMWA) mwaka jana, kilifanya tathmini ya utafiti kuhusu rushwa ya ngono kwa wanahabari katika mikoa 12, ikiwahusisha wanahabari 250, kati yao wanaume 85 sawa na asilimia 34 na wanawake 165 (asilimia 66).

Mikoa iliyoshirikishwa ni Dodoma, Tabora, Morogoro, Dar es Salaam, Mwanza, Mtwara, Lindi, Tanga, Shinyanga, Ruvuma, Mara, Arusha, Unguja na Pemba.

Tathmini ya muundo na utendaji ndani ya vyombo vya habari katika usawa kijinsia na kupinga udhalilishaji kinamama ilionyesha kwa wanawake kuna aina ya athari za matukio.

Mchanganuo wa uhalisia na idadi katika mabano ni kama ifuatavyo: Walioaliathiriwa ni 63 kwa kurubuniwa kimapenzi; mitandaoni (43); shambulio la kimwili (38); kulazimishwa kingono (31); na 12 walibakwa.

Utafiti huo unaeleza kwa waliowahi kutendewa hivyo wako 73 na walikiri kufanyiwa na bosi au maofisa waandamizi; 45 marafiki na watu wa karibu; 23 wahariri; wanne walilia na wakurugenzi na watatu wafanyakazi wenzao.

Ni utafiti ulioenda mbali kuhoji hatua zilizochukuliwa baada ya vitendo hivyo, ndipo ilipobainika kuna wanahabari 51 waliowakatalia wahusika.

Waliohojiwa wengine 40 waliwaambia marafiki zao; 38 waliwaeleza waajiri; 30 walikaa kimya; 16 waliacha kazi; na 14 waliwaambia wenzao.

Aidha, katika waliohojiwa kusumbuliwa na hatua zao; 60 walidai hakuna hatua zinazochukuliwa na utawala; 42 walihofia kuathiri kazi zao; 38 walidai kufanyiwa na wenye maradaka kikazi; 29 walihofia kutoaminiwa; 26 waliogopa kudhuriwa na wahusika; na 18 walihofia lawama.

Aidha, taasisi zilizohojiwa 51 zilisema hakuna sheria, huku 71 zinataka mafunzo yawepo kwa ngazi zote; 51 zinataka mchakato kukabiliana na rushwa ya ngono; 39 zinadai mafunzo kwa maofisa utawala na wahariri; huku 12 zinahitaji njia sahihi ya kueleza ukatili wa kijinsia.



Mwandishi wa habari mwanamama akiwa kazini.

Matarajio ya jumla kwa wanahabari hao, ni kuwapo elimu ya kutosha kuhusu unyanyasaji wa kijinsia ili kutokomeza rushwa ya ngono.

### WANAHABARI WAFUNGUKA

Agness Shayo, ni mwanamke aliyepo katika ngazi za juu za uamuzi katika chombo cha habari cha kanisa, Radio Maria, anasema kila mwanamke anaweza kufikia mafanikio pasipo bila kutoa rushwa ya ngono.

Agness ambaye ni Msimamizi Mkuu wa Vipindi vya Radio Maria, inayomilikiwa na Kanisa Katoliki, anasema muhimu ni mwanamke kujitambua, pia wajibu wake katika anachokifanya katika chumba cha habari.

Dokezo lake kwa wanajinsia wenzake, ni namna ya kutambua na kutofautisha kazi na bosi. Anafafanua: "Ukijua kazi ndio msingi wa kukufikisha katika malengo yako, utahakikisha unaongeza bidii.

"Ukijua pia bosi ni mtu mwenye mamlaka tu ambaye wakati mwingine haidumu, hutamtegemea bali utategemea kazi yako," anadema.

Anasema mwanamke anapotambua kazi inamtaka afanyike vipi, atakuwa na bidii kiasi kwamba bosi akimchukia, kazi zake zitapiga kelele kupitia wanaomzunguka.

"Ukipandishwa kwenye nafasi za juu kwa rushwa ya ngono ni wazi utashindwa kutokana na uwezo mdogo wa kiutendaji. Ina maana, unategemea mtu ili kutimiza malengo yako na siyo kutegemea kazi zako," anasisitiza Agness.

Anafafanua kuwa mwanamke anayetaka kufanikiwa katika chumba cha habari, anapaswa kutathmini namna majukumu au nafasi yake inavyoisaidia vipi kampuni kufikia malengo.

"Wito wangu kwa wanawake wanaorubuniwa, kikubwa wanapoingia kwenye sekta ya habari watambue wapo sehemu salama. Wasimamie wanachokiamini na wapende kujifunza," anasisitiza.

Khadija Mustapha, mwandishi wa habari katika blogu ya kijamii, anaueleza unyanyasaji kingono unajumuisha waandishi wa habari kushindwa kupandishwa vyeo kwa sababu ya kumkataa bosi.

"Kama ikitokea bosi anakulazimisha, njia rahisi ni kumshtaki ngazi za juu, ili kuepuka kuendelea kuishi katika unyanyasaji," anasema.

Mwanahabari mwandamizi katika gazeti jijini, Dar es Salaam, Romana Mallya, anasema kufanya kazi ya uandishi bila kutoa rushwa ya ngono inawezekana, kwa mwandishi anayejiamini.

Romana anasema, mwandishi wa habari mwanamke anatakiwa kukua kila siku kikazi kuepuka vishawishi, akiwa na ufafanuzi:

"Mwanamke atambue anaweza kutoka mwenyewe kimaisha bila ya kushikwa mkono kwa kujituma kazini, kujiamini na kuongeza bidii katika kazi zake."

Zuhura Masoud, mwandishi wa habari wa kujitegemea, anachangia mchanganuo kiufundi akiwapa angalizo waandishi wa kike wajenge uhusiano na kimapenzi na watoa taarifa ni kujiingiza katika mitengo ya magonjwa, ukiwamo Ukimwi.

Mwanahabari Grace John, anaeleza uzoefu wake wa miaka 14, kwamba kuna kumea unyanyasaji wa kingono, hata kutumika kigezo cha kumnyima mwandishi mwanamke nafasi za juu au nyeti.

"Kwa sababu umemkataa, anakukalia kimya, hakupangii kazi, hakuongeleshi, hakuulizi chochote na unaona kabisa kazi unazoweza kuzifanya anapewa mtu mwingine," anasema.

Anafafanua kwamba katika kukabiliana na magumu hayo, mwandishi mzoefu analazimika kujipangia majukumu mengine kihbari na kwa njia tofauti aonekana anafanya kazi.

Wito wa Grace, anasema waandishi wa habari vijana wanaweza kuepuka vishawishi kwa kutowakubali kimapenzi mabosi wao, ili wapendekezwe kikazi ikiwamo nafasi ya vyeo.

"Utumishi au ajira salama ni ile uliopata kwa juhudi zakom kwa sababu kama ikitokea aliyekupa ajira ya upendeleo hayupo, tambua kabisa nafasi yako itakuwa rehani," anatoa angalizo.

Rosemary Mmari, anayetumikia kituo cha runinga, anasema mwanamke yeyote anaweza kufika anakotaka kwa juhudi zake na siyo kutumia mwili wake.

Anakiri kuwashuhudia waandishi wanawake waliotumia miili yao kupandishwa vyeo, lakini wakashindwa kudumu kwa sababu hawajiwezi.

### WIZARA YA AFYA

Katika vipaumbele vya mwaka wa fedha 2021/21 vya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, vinainisha kampeni za kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto.

Inaelezwa kuwapo fedha Sh. milioni 791 zilizotengwa kwa ajili ya kuratibu kampeni za kutokomeza ukatili dhidi ya wanawake na watoto nchini.

**Makala hii imeandaliwa ikiwa katika mfumo wa ripoti ya kitafiti.**

# KANALI MAHAMADY DOUMBOUYA

## ●Maisha yake yamejaa utata, usiri, ubabe
## ●Rais Conde alimwamini, akampindua kiulaini



Rais Alpha Conde, akiwa ndani ya gari ya jeshi akipelekwa sehemu isiyojulikana. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

**Na Mwandishi Wetu**

JINA la Kanali Mahamady Doumbouya, limepata umaarufu wa ghafla, baada ya kufanikiwa kufanya mapinduzi yasiyomwaga damu nchini Guinea.

Mapinduzi hayo ya kushtukiza ya kijeshi yamemaliza hatamu ya kiongozi mkongwe barani Afrika, Alpha Conde, ambaye uongozi wake ulitawaliwa na utata.

Kanali Doumbouya, alikuwa kiongozi wa kikosi maalum cha kumlinda Conde, kilichofahamika kama GFS, na jina lake halikuwa likijulikana sana.

Conde mwenye umri wa miaka 83, alifanya jaribio la kubadilisha katiba na kuruhusiwa kuongoza Guinea kwa muhula wa tatu uliogubikwa na maandamano na ukandamizaji dhidi ya upinzani.

**KIKOSI CHA GFS**

Kikosi maalum cha kumlinda Rais Conde, kiliundwa kwa ajili ya kumkinga kiongozi huyo dhidi ya wapinzani wake.

Kanali Doumbouya, aliaminiwa kuongoza kikosi hicho baada ya kuitwa na kiongozi huyo kutoka Ufaransa ambako alikuwa akitumikia jeshi la nchi hiyo.

Wakati anaongoza GSF, ilikuwa vigumu kuguswa na mtu yeyote na hata matumizi ya pesa haikuruhusiwa kukaguliwa.

**MAPINDUZI YA GHAFLA**

Pamoja na Rais Conde, kuwaamini wanajeshi wa kukosi hicho, Septemba 5, mwaka huu, kilimgeuka na kumwondoa madarakani baada ya kuipindua serikali yake.

Kabla ya mapinduzi hayo, kuripotiwa kwa ufyatulianaji wa risasi karibu na makazi ya rais katika mji wa Conakry.

Kamanda wa GFS, Kanali Doumbouya, alijitokeza hadharani na kuthibitisha kuchukua serikali kupitia runinga ya serikali na kuahidi kusimamia mabadiliko ya serikali kwa njia ya amani.

"Ubinafsishaji wa maisha ya kisiasa umekwisha. Tutaweka mpango wa mpito ulio wazi na unaojumuisha watu wote. Tutaweka mfumo ambao sasa haupo," alisikika Doumbouya akisema wakati huo akiwa amezungukwa na maofisa wa GFS, waliobeba silaha na kujifunika bendera ya Guinea.

Kanali Doumbouya, kuanzia hapo ndipo alipoanza kuongoza nchi hiyo kupitia kamati inayoitwa National Committee for Rally and Development (CNRD).

**CHANZO CHA PICHA**

Kwa ujumla mataifa ya Afrika Magaharibi, yamepata ugumu na hawajui nini kitakachotokea baada ya mapinduzi hayo, kutokana na mtu aliyeshika madaraka kutofahamika na hata falsafa zake zimekuwa vigumu kujulikana.

Pamoja na Jumuiya ya Kiuchumi ya Mataifa ya Afrika Magharibi (ECOWAS), kulaani mapinduzi hayo, imetuma ujumbe maalumu kwenda nchini humo kuzungumza na kiongozi huyo kujua hatima ya kiongozi wa zamani pamoja na urudishwaji wa katiba ya nchi.

Mapinduzi nchini Guinea yanaonekana kuchchewa na majibu dhaifu kwa matukio kama hayo katika nchi jirani za Mali na Chad, na kueleza udhaifu wa kisiasa na usalama wa nchi za Afrika Magharibi na Kati.

**MAISHA YA USIRI**

Maisha ya Kanali Doumbouya, yamegubikwa na usiri kiasi ambacho mambo mengi yanayomuhusu hayajulikani sana hasa maisha ya utotoni.

Kinachofahamika ni kabila analotoka la Malinke ambalo ni la Rais Conde, pia anatoka Mkoa wa Mashariki wa Kankan wa Guinea.

Kuna taarifa kuwa aliishi Forecariah, magharibi mwa Guinea, ambapo alihudumu kama ofisa uchunguzi na huduma za kijasusi.

**MAFUNZO YA KIJESHI**

Doumbouya anaripotiwa kuhudhuria Chuo cha mafunzo ya kivita jijini Paris, nchini Ufaransa.

Ana uzoefu wa miaka 15 wa kijeshi ambayo ni pamoja na kuhusika katika operesheni nchini Afghanistan, Ivory Coast, Djibouti na Jamhuri ya Afrika ya Kati.

Pia muda fulani alihusika na ulinzi wa watu mashuhuri katika nchi za Israeli, Cyprus, Uingereza na Guinea.

Inasemekana kazi zote alikamilisha vyema.

Pia alipata mafunzo ya wataalamu wa ulinzi wa kiutendaji katika Chuo cha Usalama cha Kimataifa huko Israeli, kozi ya mafunzo ya makamanda wa kijeshi nchini Senegal, mafunzo ya ofisa msimamizi Chuo cha Staff College Libreville (EEML) cha Gabon na Chuo cha Vita huko Paris.

Alikuwa kama mwanajeshi wa kigeni yaani 'legionnaire' katika Jeshi la Ufaransa hadi mwaka 2018 wakati Conde alipomtaka arudi Guinea kuongoza GFS, iliyoanzishwa mwaka huo.

**JE, FAMILIA YAKE INAJULIKANA?**

Kiujumla hakuna anayeijua familia ya Kanali Doumbouya, lakini inaaminika ameoa mwanamke wa Kifaransa na ana watoto watatu.

**ONYO MTU ASIYEAMINIKA**

Mwaka 2018, kulitolewa ripoti kadhaa kwenye vyombo vya habari vya Guinea zikitilia shaka sifa za Doumbouya.

Mnamo Oktoba 2018, Le Guepard aliwaonya watu wa nchi hiyo kuwa ipo siku watashuhudia kuanguka chini ya ulimi mtamu wa mtu atakayewanyonga siku za usoni.

Mnamo Agosti 2021, Friaguinee lilidai kwamba Dombouya alinyimwa uraia wa Ufaransa kwa sababu mwenendo wake ulionekana kuwa kinyume na maadili na kanuni za Jeshi la Ufaransa.

Wakati iliripoti kuhusu mali kadhaa zinazodaiwa kuwa ni za kanali Doumbouya, na kuuliza ofisa huyo wa kijeshi, ambaye alikuwa akipokea mshahara wa kila mwezi wa chini ya faranga milioni tano, anawezaje kujenga majengo mengi ya kifahari?

Hata hivyo, mwezi Mei, mwaka huo, Doumbouya alikuwa miongoni mwa maofisa 25, waliolengwa kwa vikwazo vya Umoja wa Ulaya (EU) kutokana na ukiukwaji wa haki za binadamu. Lakini vikwazo hivyo vilifutwa haraka.



Kiongozi wa mapinduzi ya Guinea, Kanali Mahamady Doumbouya.

**HABARI KIMATAIFA**

## Kenya, Estonia kushirikiana kukuza uchumi wa nchi zao

**Nairobi,** KENYA

RAIS Uhuru Kenyatta amefanya mazungumzo na mwenzake wa Estonia Kersti Kaljulaid ambaye yuko Kenya kwa ziara rasmi ya siku tatu.

Wakati wa majadiliano, viongozi hao wa nchi mbili walishuhudia kusainiwa kwa mpango kazi wa pande mbili wa ushirikiano juu ya ushauri wa kisiasa, afya na pia kutia saini barua yenye azimio la kimazingira. Viongozi hao wawili walionyesha kuridhika na ushirikiano uliopo kati ya nchi hizo mbili katika sekta mbalimbali haswa Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) na uvumbuzi, nchi ya Estonia inasifiwa sana kama mfano mwema duniani.

Uhuru alimshukuru Kaljulaid kwa kuandamana na ujumbe wa ngazi ya juu wa kibiashara kushiriki katika Jukwaa la Biashara kati ya Kenya na Estonia kwa kuzingatia huduma za elektroniki.

Viongozi hao wawili walisisitiza kujitolea kwao kuendelea kuimarisha ushirikiano wa pande mbili katika sekta mbalimbali kama biashara na uwekezaji na hata mabadiliko ya kidijitali kwa lengo la kuhuisha ukuaji wa uchumi ili kutengeneza ajira kwa vijana wa Kenya. **BBC**

## Jeshi Guinea lafungia akaunti zote za serikali

**Conakry,** GUINEA

MAMLAKA ya kijeshi ya Guinea, imeamuru benki kufungia akaunti zote zinazohusiana na serikali ili kupata mali za serikali.

Jeshi ambalo lilishika udhibiti wa nchi hiyo mwishoni mwa wiki iliyopita, linasema agizo hilo linaathiri akaunti za taasisi na watu binafsi wa serikali inayomaliza muda wake.

Maofisa wa juu wa serikali ya Rais aliyeondolewa madarakani Alpha Condé hawataweza kutumia akaunti zao.

Viongozi wa mapinduzi walichukua madaraka Jumapili na walisema wanataka kumaliza ufisadi uliokithiri, ukiukwaji wa haki za binadamu na usimamizi mbaya.

Jumuiya ya Kiuchumi ya eneo la Magharibi mwa Afrika (ECOWAS) ambayo inataka katiba kufuatwa, imetuma ujumbe wa kutaka kufanya mazungumzo na mamlaka ya Guinea.

Jumuiya hiyo imetaka Rais Condé ambaye ameshikiliwa na jeshi kuachiwa huru.

**BBC**

# Huduma za umma zakosekana Cabo Delgado na kuzua hofu

**Cabo Delgado,** MSUMBIJI

TAASISI zote za serikali Msumbiji Kaskazini mwa Jimbo la Cabo Delgado bado zimefungwa, takribani mwezi mmoja baada ya shambulio la kigaidi katika eneo hilo kudhibitiwa.

Hali hiyo inachukuliwa kuwa mbaya katika Wilaya ya Palma, eneo pekee ambalo raia wameruhusiwa kufika kati ya maeneo kadhaa ambayo yamekombolewa kutoka kwa wanajihadi na vikosi vya pamoja vya Msumbiji na Rwanda.

Watu wachache ambao walikuwa na ujasiri wa kurudi kwenye nyumba zao wamekuta vitu vyao vimeharibiwa na ulinzi mkubwa wa jeshi.

"Nilikimbilia Quitunda na niliporejea kijiji cha Palma, yapata wiki moja iliyopita, niliwakuta wanajeshi na majengo yote ya serikali yakiwa yameharibiwa na kufungwa," alisema Sufo Assane, miongoni mwa watu waliorudi mapema.

Licha ya kutokuwapo kwa taasisi za serikali, familia nyingi zilizorejea katika eneo lililokumbwa na shambulio wanakabiliwa na tatizo la njaa na wanaishi kwa kutegemea mazao ya wengine ambao waliweza kulima.

"Tangu tuwasili hapa, hatujapokea msaada kutoka serikalini na tunakula mihogo, kisamvu na matembele ambayo tunapewa kutoka kwa watu walioweza kufanikiwa kupata katika mashamba yao," Bacar Macotcha alieleza.

Baadhi ya wafanyabiashara wadogo wameanza kufanya biashara zao kwa kuuza bidhaa muhimu kama chakula, lakini wana wateja wachache kwa kuwa familia nyingi hazina fedha.

Wasiwasi mwingine upo kwenye malazi, baadhi ya familia nje bado wakiwa wanasubiria fursa ya kujengewa nyumba zao ambazo ziliharibiwa.

Watu wamekuwa wakilaumu kuhusu suala la kukosekana kwa kituo cha afya katika eneo la Palma.

"Hospitali imefungwa na hakuna wahudumu wa afya, mtu akiugua inabidi waende Quitunda, ambako ni takribani kilomita 15 (9miles) kutoka hapo," alisema Aissa Momade. **BBC**



Picha iliyochukuliwa na meli ya ulinzi wa Italia ya Guardia Costiera, ikimwonyesha mwokoaji akisaidia kuwaokoa wahamiaji wawili Bahari ya Pwani ya Lampedusa karibu na Kisiwa cha Conigli juzi. **PICHA: AFP**

# 3% pekee Afrika wamechanjwa chanjo corona

**New York,** MAREKANI

WAKATI Afrika ikiwachanja watu wake kwa asilimia tatu, COVAX ina mpango wa kupunguza dozi ya chanjo ya corona barani.

Mataifa ya Afrika yatapokea zaidi ya dozi milioni 100 za chanjo ya Covid-19 zaidi ya kile wanachopokea kutoka mpango wa chanjo wa COVAX kufikia mwishoni mwa mwaka, Shirika la Afya Duniani (WHO), limesema.

Afrika ilikuwa inapokea dozi milioni 520 kufikia mwezi Desemba.

Hivyo kwa upande wa COVAX, wameweza kupata zaidi ya dozi milioni tano, kwa mujibu wa WHO.

Mpango wa Umoja wa Mataifa (UN) wa dunia unasema mkataba wa pande zote mbili wa mataifa ambayo yanatengeneza ambayo yenye mataifa tajiri pamoja na sheria za kudhibitisha zinalaumiwa kuwa sehemu ya kupunguza malengo yaliyowekwa.

Wakati chanjo ilipokuwa inasambazwa katika mataifa ya Afrika, angalizo lilitolewa na COVAX kuwa hakuna dalili ya usawa, jitihada za dunia za kutaka chanjo kutolewa kwa usawa bado haijazaa matunda.

Mataifa ya Afrika kwa kiwango kikubwa wanategemea COVAX, mpango huo wa unashindwa kutoa chanjo kama ilivyoahidi.

Zaidi ya mataifa 54, ni mataifa 12 peke yake ndio yamefikia malengo ya dunia kwa kuwapa chanjo watu wake kwa asilimia 10 ifikapo mwishoni mwa Septemba.

Na taarifa kuwa baadhi ya mataifa tayari yameanza kupewa dozi za nyongeza licha ya wito kutolewa wa kutaka wasifanye hivyo mpaka mwishoni mwa mwaka, serikali za Afrika zinapaswa kufikiria namna ya kupata chanjo kwa ajili ya watu wake.

Ni asilimia tatu tu ya watu wa Afrika wamepata chanjo kuliko na zaidi ya watu bilioni moja. **BBC**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

**MATANGAZO MCHANGANYIKO**

PATA MKOPO WA HARAKA KWA MASHARTI NAFUU KUTOKA ENTEPRISES FINANCE LIMITED (EFL).
KWA MAWASILIANO ZAIDI
**TUPIGIE:0677 111 333**
**AU 0758 112 332**

**OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676**

## KUPOTEA KWA CHETI



**BENJAMEN KIMAMBO** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba S.0475/0036 kilichotolewa na **KIDIA SEKONDARI** mwaka **1999**. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi.
**Taarifa ya polisi: MOS/RB/730/2010**.

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**FLORIAN NESTORY NJUNWA** ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YAKE YA GARI YENYE NAMBA ZA **USAJILI T 251 BTF. CHASSIS NAMBA MR 515604323. ENGINE NAMBA M13A1115442.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **DAR/URA/RB/441360/2021.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**SADAT BARAKAT SALEH** ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YAKE YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 171 BSP.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **DAR/BUG/RB/440261/2021.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**MOHAMMED AMOUR DUGHEISH** ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YAKE YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 837 CQA.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **DAR/BUG/RB/440788/2021.**

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika Mahakama ya Mwanzo**
**MJINI MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi**
**NO.285/2021**

Ombi la **SAMIA MTORO MKUDE** kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya marehemu **ISMAIL ATHUMAN**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo **tarehe 13/09/2021** kabla huyo mwambaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa.

Sahihi ya Hakimu
HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO MJINI
MOROGORO

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika Mahakama ya Mwanzo**
**MJINI MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi**
**NO.279/2021**

Ombi la **FANUEL MUKAMA TANDA** kuteuliwa msimamizi wa mirathi ya marehemu **PHILIMON BARAOYE MKAMA TANDA**
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo **tarehe 12/10/2021** kabla huyo mwambaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa.

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**NDUMI FELEMON KWEKA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA HIACE COMMUTER** yenye namba za usajili **T 718 DCZ. Chassis No. RZH1331002363, Engine No. 2RZEAA2363.**Yeyote atakae iona atoe taarifa kituo cha polisi.
Taarifa ya polisi **DOD/DOD/RB/441855/2021.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**CONSOLATHA DEUSDEDIT KADIKILO** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA HARRIER** yenye namba za usajili **T 826 DLG. Chassis No. ACU300020561, Engine No. 2AZ1481408.**Yeyote atakae iona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi **DOD/DOD/RB/440182/2021.**

## KUPOTEA KWA KADI YA TREKTA

**PASCHAL JOSEPH DUWAY** anatangaza kupotea kwa kadi ya Trekta aina ya **TRECTOR FORD** yenye namba za usajili **T679DDT,** Chasisi namba **EA314C5G08BA60702,** Engine namba **E497537.** Yeyote atakayeiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi Taarifa: **MAN/BAB/RB/438126/2021.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**FALY DEAL AUTO PVT LTD** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki yenye namba za usajili **MC 693 BUP** aina ya **BOXER.** Yeyote akaeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo jirani yake.
Taarifa ya Jeshi la Polisi **MAJ/RB/1588/2021.**

**MAHAKAMA YA HAKIMU MKAZI**
**MWANZA**
**WILAYA YA NYAMAGANA MWANZA**
**SHAURI LA MIRATHI NO 17/2021**
**MWOMBAJI............JUDITH KANZANILA**
**MAREHEMU......GERAL OTIENO NJURA**

**KWA: YEYOTE ANAEHUSIKA**

**KUITWA SHAURINI**
Mwombaji tajwa hapo juu amefungua shuri la mirathi ya marehemu **GERAL OTIENO NJURA** katika mahakama hii hati za mirathi zinapatikana katika mahakama hii.
Tunaomba yeyote mwenye pingamizi katika mirathi hii anatakiwa kuhudhuria mahakamani tarehe 01/10/2021 saa 2:00 asubuhi ninyi/ wewe binafsi au wakili wenu kisheria.
**Zingatia** kwamba kutohudhuria kwenu kwa tarehe tajwa, kesi hii itaendelea bila nyinyi kuwepo mahakamani.
Imetolewa kwa mkono wangu na muhuri wa mahakama hii leo tarehe 06/09/2021.

HAKIMU MKAZI
WILAYA YA NYAMAGANA
MWANZA

**HAKIMU MKAZI**
**WILAYA YA NYAMAGANA.**
**MWANZA**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA RUFANI YA TANZANIA**
**ILIYOPO ARUSHA**
**SHAURI LA MAOMBI YA MADAI**
**NA. 492/01 YA 2019**
**CATHERINE HONORATI...............MLETA MAOMBI**
**DHIDI YA**
**1. CRDB BANK**
**2. METHOD KAUNGA MORIS**
**3. HONORATI BIASHARA JOHN LYOMBE.............WAJIBU MAOMBI**

**KWA:**
**1. METHOD KAUNGA MORIS**
**2. HONORATI BIASHARA JOHN LYOMBE**

**POPOTE MLIPO**
Mnajulishwa kwamba shauri la maombi ya madai tajwa hapo juu limepangwa kusikilizwa na Mahakama hii Arusha tarehe 29 Septemba, 2021 saa tatu kamili asubuhi (3:00). Mnapaswa kuhudhuria siku na tarehe iliyopangwa bila kukosa na endapo hamtahudhuria nyinyi wenyewe au wawakilishi wenu wanaotambulika kisheria basi maombi yatasikilizwa bila ya uwepo wenu.
Imetolewa kwa Amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 26/08/2021.

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**FLORIAN NESTORY NJUNWA** ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YAKE YA GARI YENYE NAMBA ZA **USAJILI T 251 BTF. CHASSIS NAMBA MR 515604323. ENGINE NAMBA M13A1115442.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **DAR/URA/RB/441360/2021.**




**NJOO UTANGAZE**
**BIDHAA YAKO**
**KWA BEI NAFUU SANA**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

TOM alipooa alidhani kuwa ataishi kwa amani, furaha na kupata utulivu kama inavyokuwa kwa rafiki na wenzake wote waliofanya hivyo.

Siku zote ndoa ni masikilizano, maelewano, na anayeoa hupata furaha na heshima. Kinyume chake, kwake imekuwa ni misukosuko, mikosi na balaa. Badala ya kuwa ndoa yenye furaha, akajiingiza kwenye mtego hatari ambao hata baada ya kuufahamu, hakuweza kuutegua tena. Alichelewa. Ukawa ni mwanzo ni vilio, maafa na mtiririko wa mambo ya kushangaza.

Hebu pata kila nakala ya gazeti hili kufuatilia kisa hiki cha kushangaza na kusikitisha.

# Namsaka mke wangu-**10**

**Mtunzi anapatikana (0716 350534)**

**Na Adam Fungamwango**

ALIKUWA hajaelewa kuwa ni kweli Tom ataondoka naye au anamtumia, lakini akimaliza atatoroka, na huenda akamdhuru Sam na kumrudia mkewe Farida.

Pamoja na yote aliamua kujaribu bahati yake.

"Kama ikishindikana akinitoroka na mimi nitatoroka na kurudi kwetu Manyoni." Alijiambia.

"Kumbuka, ukimuwekea hiyo dawa, usichukue kila kitu. Tafuta vitu ambavyo vinaweza kunisaidia mimi kupata ninachokihitaji. Na hiyo itakuwa ndiyo salama ya kutokukugusa. Nadhani nimeshakwambia kila kitu. Kilakinachonihusu na mke wangu unakijua. Tena nimekumbuka, hata simu yake chukua, halafu tutajua baadaye."

"He baba, sawa, ila umenipa mzigo mzito, maana mimi umenifanya sasa kama polisi mpelelezi."

"Ndiyo utaanza taratibu kujifunza."

"Enhee, kitu gani cha kwanza kinatakiwa?"

"Twende mjini kwanza. Nikakununulie nguo nzuri za gharama. Halafu tupitia saluni, usuke mtindo ambao wewe ukisuka unakupendeza sana. Yaani leo jioni uwe kama malaika. Akikuona atababaika. Ila la muhimu. Akisema twende nyumba ya wageni, kataa kwa sababu huko hatutopata kitu tunachohitaji, hata kama utamuwekea dawa."

"Nimekuelewa hani. Leo kwa Mwenda watanikoma, naingia siyo baamedi tena. Naingia kama msichana mrembo nitakayetetemesha baa nzima." Alijigamba na baadaye akauliza "Wewe nawe vipi?"

"Mimi nitarudi kwenye sura yangu ile ulioiona mara ya kwanza."

*****************************

Kila kitu kilienda kama kilivyopangwa. Siku iliwadia. Shopingi ilifanywa. Tedi alipelekwa saluni. Akapambwa akapambika. Akavaa akang'aa. Tom naye hakuwa nyuma. Alipiga pamba zake, ambazo alidhani kuwa zingempendeza. Kiasi alipendeza. Kila aliyemtazama mwenzake alicheka. Akampongeza kuwa amependeza.

Waliongea mengi. Wakafanya mengi. Lakini kila mmoja alikuwa na lake moyoni alilofikiria. Ni kuhusu kazi wanayokwenda kuifanya. Na haswa Tedi. Kwake ilikuwa ni kazi ngumu. Ni kwa vile mtu aliyemtuma kwa siku chache tu, ambazo amekaa naye aligundua kuwa ni mtu mzuri. Mkarimu. Mcheshi na mwenye huruma. Ni tofauti na mwanzo alivyofikiria. Alianza kumshangaa mwanamke mwenzake Farida kumtoroka mwanaume wa aina hiyo, wiki moja tu baada ya ndoa. Awali alidhani kuwa huenda ni mwanamke katili, mnyanyasaji.




Pamoja na hayo aliwaza kuwa kuna baadhi ya wanaume huficha makucha yao wanapopata wanawake wapya. Au mwanzoni mwa mapenzi. Baadaye wanakuja kuonyesha tabia yao halisi.

Licha ya yote hakutaka kumpoteza. Tayari walishapanga mipango mingi, ikiwamo kumlipia ada ya shule ya urembo. Hilo alikuwa na uhakika nalo. Yaliyobaki alimuachia Mungu.

Waliingia kwenye baa ya Mwenda. Macho ya watu wengi yalikuwa kwake. Kila mmoja alimshangaa Tedi.

Tedi huyu huyu ambaye ni baamedi kwenye baa ile. Hakuwa Tedi yule tena wanayemfahamu. Kwa siku chache amekuwa adimu kwenye baa hiyo. Awali alipoingia si wengi waliomfahamu.

Pamoja na kwamba Tedi ni msichana mrembo, lakini ulizidi kwa siku chache baada ya kuwa na Tom.

Tom hakumuacha kurudi tena kufanya kazi yake ya zamani. Alimtumia kwa kampani. Pamoja na kazi nyingine, ambayo amempa kuifanya.

Hata baadhi ya wenzake, ikiwamo yule ambaye alimfanyia mipango kuwa na Tom walianza kumuonea wivu. Walijua ni msichana mzuri. Lakini hawakuwahi kufikiri kuwa kumbe Tedi ni mrembo zaidi kuliko walivyodhani.

Walikwenda kuketi kwenye siti, ambayo ilikaribia siku ile ya kwanza walipokaa. Wakaagiza vinywaji. Walianza kunywa kwa furaha kama mtu na mpenzi wake. Ilikuwa ni zaidi ya siku ile ya kwanza. Sasa hivi wameshazoena. Robo saa baadaye Sam aliingia. Tom na Tedi mawazo yake walijua kuwa angeambatana na Farida kama ilivyokuwa siku ile au zingine nyuma. Haikuwa hivyo. Alikuwa peke yake. Wasiwasi wa kwenda na Farida ndiyo ulimfanya Tom kubadili sura yake kama anavyofanya siku zote.

Kwa mbali alianza kuingia na furaha. Aliona kutokuwapo kwa mkewe Farida kungeweza kurahisisha kazi au mpango mkakati alioupanga.

"Leo inaweza kuwa vizuri zaidi, kwa sababu hana mwanamke, anaweza kunitongoza akataka niende naye." Tedi alimnong'oneza Tom.

"Na ndiyo maana ninafanya haya yote." Alijibu Tom na kuona mawazo yake yanafanana na Tedi.

"Kilichobaki toka hapa nenda kapite pale karibu yake, tembea kwa madaha kuelekea msalani hadi akuone, halafu tuone nini kitaendelea."

Tedi alinyanyuka. Kwa madaha ya kike alianza kupiga hatua moja kwa mpangilio maalum. Alipita mbele ya meza aliyokuwa amekalia Sam. Mwanaume ambaye ndiye anayeonekana kuongozana na Farida, mke wa Tom, aliyemtoroka wiki moja baada ya harusi."

"Tedi hakumchanganya Sam pekee. Wanaume wengi ndani ya baa walionekana kunyanyasika na urembo wa ghafla wa Tedi. Macho yote yalikuwa kwake.

**Licha ya yote hakutaka kumpoteza. Tayari walishapanga mipango mingi, ikiwamo kumlipia ada ya shule ya urembo. Hilo alikuwa na uhakika nalo. Yaliyobaki alimuachia Mungu.**

Haikupita hata dakika moja, Sam alisimama. Alionekana kama kuna mtu anamtazama. Halafu akaanza kutembea kuelekea msalani. Kwa ramani ya baa ile au baa nyingi nchini. Vyoo vya wanaume na wanawake wala haviwi mbali sana. Vinapeana migongo tu au milango tofauti.

Alikoelekea Sam ni kule kule tu alikoelekea Tedi. Kwa jicho la tatu, Tom alijua Sam anamfuata Tedi. Anataka kumvizia akitoka msalani amwambie jambo. Hadi wakati huo alikuwa anafuahia mpango wake kuwa unaelekea vizuri.

Hakutaka kuangalia zaidi. Alijua Tedi atakuja kumweleza kila kitu kilichoendelea. Aliendelea kupiga kinywaji. Muda si muda Tedi alirejea na tabasamu mdomoni.

"Vipi, mbona umefurahi sana."

"Mhhh, rafiki yako huyo."

"Nani?"

"Sam. Si kanisimamisha. Akaniambia umempata buzi siku hizi anakupendezesha, basi sisi unatuona takakata."

Tom alicheka kicheko kifupi. "Yaani mimi nimeshakuwa buzi?"

"Anakuita buzi. Akanikumbushia siku ile nilikutongoza ukanitolea nje, kwa sababu ya yule mwanamke, leo hayupo, unasemaje. Nikamwambia yaani nimuache bwana yangu pale niondoke na wewe, inawezekana kweli. Akaniambia hata kesho. Nikamuuliza yule mwanamke wako vipi? Akaniambia amekwenda Dar es Salaam kwa ndugu zake atarejea baada ya siku tatu kuanzia leo."

"Enhee halafu?"

"Nikamwambia basi tufanye kesho. Akaniomba namba ya simu nikampa. Lakini nikamwambia mimi masuala ya kunipeleka kwenye nyumba ya wageni sitaki. Kama unanihitaji basi iwe kwako. Na nikamdanganya kuwa kesho sitaki awepo kwenye baa hii, twende kwingine, kwa ajili ya kukukimbia wewe, ili usitukute. Yote amekubali."

Tom alimkumbatia na kumbusu Tedi. Yaani we mwanamke. Tayari umeshafika huko. Umeongeza na mengine ambayo hayakuwepo, lakini yana msaada sana."

Wakati huo, Sam alikuwa anatupa jicho la wizi akiona Tom alimkumbatia Tedi, lakini hakujua kama walikuwa wakimsema yeye.

"Kesho mimi siondoki kabisa kule tunapoishi. Wewe nenda naye huko. Hakikisha anakunywa pombe na nyingine mnaondoka nayo, ili iwe rahisi kumwekea vidonge. Usikosee kitu chochote. Halafu usiruhusu akushikeshike sana..."

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

CHEZA USHINDE JACKPOT TZS. 482

MECHI KALI
HOME
AWAY
MANCHESTER UTD
1.25 | 6.10 | 10.78
NEWCASTLE

1 WEKA PESA.
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4 - WEKA PESA.
vodacom m-pesa airtel money tigo pesa EZYPESA
- FUNGUA MENYU YA HALOPESA
- CHAGUA LIPA/LIPIA BILI
- WEKA NAMBA YA KAMPUNI 150888, KUMBUKUMBU 888.
- KISHA WEKA 500 AU ZAIDI.
SEND
halopesa

2 WEKA BET.
- PIGA *150*87#
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249
18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA: 0764115588, 0677115588 0685115588
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# HAALAND, REAL MADRID WAFIKIA MAKUBALIANO



**MADRID,** Hispania

KLABU ya Real Madrid imeripotiwa kuwa imefikia makubaliano ya kumsajili Erling Braut Haaland kwa mazungumzo pekee.

Mshambuliaji huyo raia wa Norway aligonga vichwa vingi vya habari za uhamisho wakati wa uhamisho wa msimu wa majira ya joto, lakini Borussia Dortmund waliweza kusalia naye.

Hata hivyo, dau la pauni milioni 68 la kumnunua Haaland linaweza kuanza kutumika msimu ujao wa majira ya joto, linaendelea kuwaweka karibu wanunuzi wenye nia na saini ya nyota huyo.

Klabu za Real Madrid, Manchester City, Manchester United, Paris Saint-Germain na Bayern Munich zinatajwa pia kuwania saini ya nyota huyo.

Kuna taarifa kuwa hatima ya nyota huyo tayari imeshaamuliwa kati ya Real Madrid na Dortmund juu ya uhamisho wake kipindi cha msimu ujao wa majira ya joto.

Real Madrid waliambiwa kuwa wasingeweza kumpata Halaand katika dirisha lililopita, lakini sasa wana nafasi kubwa.

Haaland alifanikiwa kuona lango mara 63 na kutoa pasi za mwisho 18 kwenye mechi 64 alizocheza akiwa na Borussia Dortmund.

# Hatima ya Dembele mbioni kuamuliwa

**BARCELONA,** Hispania

HATIMA ya Ousmane Dembele inaweza kuamuliwa hivi karibuni, kwa mujibu wa Rais wa Barcelona, Joan Laporta.

Katika utambulisho wa Luuk de Jong kama nyota wa mwisho kusajiliwa Barcelona, Laporta ameamua kugusia hatima ya nyota huyo juu ya mazungumzo ya mkataba mpya wa Dembele.

Nyota huyo wa Ufaransa kwa sasa yupo nje ya uwanja akiuguza jeraha, na amepewa jezi namba saba pale Camp Nou.

Laporta amesema amehakikishiwa kuwa mkutano na mawakala wa nyota huyo unaandaliwa ili kuweka sawa suala lake la mkataba mpya.

Rais huyo hana wasiwasi na uhusiano wao na Dembele, anaamini kuwa anafurahia kuwapo Barca, na anahisi kupendwa na klabu, hivyo angependa suala hilo liendelee.

Dembele alikuwa na mchango mkubwa katika kikosi cha timu ya Taifa ya Ufaransa kwenye michuano ya Euro 2020.



## HABARI MICHEZO

,274,020

JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE 13

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 11/09/21 | 17:00 | Brentford vs Brighton | 2.72 | 3.12 | 2.72 |
| 02. 11/09/21 | 17:00 | Watford vs Wolverhampton | 3.27 | 3.17 | 2.30 |
| 03. 11/09/21 | 17:00 | Southampton vs West Ham | 2.87 | 3.42 | 2.42 |
| 04. 11/09/21 | 17:15 | Ternana vs Pisa | 2.46 | 3.07 | 2.92 |
| 05. 11/09/21 | 19:00 | Napoli vs Juventus | 2.56 | 3.46 | 2.66 |
| 06. 11/09/21 | 22:00 | Amorebieta vs Burgos | 2.42 | 2.95 | 3.10 |
| 07. 12/09/21 | 14:00 | Montpellier vs St Etienne | 2.44 | 3.38 | 2.79 |
| 08. 12/09/21 | 16:00 | Bordeaux vs Lens | 3.09 | 3.39 | 2.24 |
| 09. 12/09/21 | 16:00 | Brest vs Angers | 2.65 | 3.30 | 2.60 |
| 10. 12/09/21 | 16:00 | Spezia vs Udinese | 2.92 | 3.38 | 2.40 |
| 11. 12/09/21 | 17:15 | Osasuna vs Valencia | 2.51 | 3.07 | 3.02 |
| 12. 12/09/21 | 18:30 | VfL Bochum vs Hertha BSC | 2.93 | 3.23 | 2.41 |
| 13. 12/09/21 | 19:15 | Ponferradina vs Almeria | 2.80 | 3.30 | 2.41 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAMOSI - 11 - SEPTEMBA 2021

| TAREHE | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:30 | 5025 | Crystal Palace vs Tottenham | 4.11 | 3.46 | 1.91 |
| 16:30 | 1316 | Hoffenheim vs Mainz | 2.04 | 3.72 | 3.28 |
| 16:30 | 2731 | Union Berlin vs Augsburg | 1.70 | 3.88 | 4.57 |
| 16:30 | 4453 | SC Freiburg vs FC Koln | 2.10 | 3.63 | 3.19 |
| 16:30 | 5106 | Greuther Furth vs VfL Wolfsburg | 5.18 | 4.29 | 1.57 |
| 16:30 | 5254 | Bayer Leverkusen vs Borussia Dortmund | 2.98 | 3.83 | 2.14 |
| 17:00 | 1940 | Arsenal vs Norwich City | 1.58 | 4.19 | 5.51 |
| 17:00 | 2027 | Celtic vs Ross County | 1.13 | 7.69 | 15.78 |
| 17:00 | 2051 | Manchester Utd vs Newcastle | 1.25 | 6.10 | 10.78 |
| 17:00 | 3125 | Leicester vs Manchester City | 4.94 | 3.90 | 1.68 |
| 17:00 | 3313 | Watford vs Wolverhampton | 3.32 | 3.12 | 2.31 |
| 17:00 | 3373 | Dundee FC vs Livingston | 2.25 | 3.20 | 3.15 |
| 17:00 | 4474 | FC Metalist 1925 vs Dynamo Kiev | 9.68 | 5.61 | 1.23 |
| 17:00 | 4597 | Brentford vs Brighton | 2.82 | 3.07 | 2.67 |
| 17:00 | 4598 | Swansea vs Hull City | 2.14 | 3.35 | 3.40 |
| 17:00 | 5245 | Bournemouth vs Barnsley | 1.82 | 3.46 | 4.25 |
| 17:00 | 5725 | St Mirren vs Dundee Utd | 2.32 | 3.06 | 3.16 |
| 17:00 | 5971 | Southampton vs West Ham | 2.82 | 3.42 | 2.45 |
| 17:30 | 3800 | Pacos Ferreira vs Sporting Braga | 4.14 | 3.45 | 1.84 |
| 17:30 | 5712 | Twente vs Utrecht | 3.55 | 3.50 | 1.97 |
| 18:00 | 1041 | Paris St Germain vs Clermont Foot | 1.35 | 5.17 | 7.75 |
| 18:00 | 2814 | WSG Wattens vs RB Salzburg | 7.96 | 5.63 | 1.26 |
| 18:00 | 3181 | Baroka FC vs Maritzburg Utd | 2.59 | 2.98 | 2.79 |
| 18:00 | 3917 | Rapid Vienna vs Admira Wacker | 1.37 | 4.74 | 6.39 |
| 19:00 | 2719 | Napoli vs Juventus | 2.43 | 3.41 | 2.86 |
| 19:00 | 3402 | Stabaek vs Viking | 3.11 | 3.65 | 2.08 |
| 19:00 | 4712 | Spartak Moscow vs FK Khimki | 1.49 | 4.13 | 6.10 |
| 19:00 | 5044 | FC Luzern vs Grasshoppers | 1.99 | 3.75 | 3.26 |
| 19:00 | 5162 | Lillestrom vs Brann | 1.58 | 4.03 | 5.11 |
| 19:30 | 2291 | RB Leipzig vs Bayern Munchen | 2.98 | 3.78 | 2.15 |
| 19:30 | 4226 | Levante vs Rayo Vallecano | 2.08 | 3.41 | 3.56 |
| 19:30 | 4416 | Chelsea vs Aston Villa | 1.32 | 5.22 | 9.64 |
| 19:45 | 1564 | Cambuur vs GO Ahead Eagles | 1.72 | 3.74 | 4.42 |
| 19:45 | 3425 | PEC Zwolle vs Ajax | 11.83 | 6.90 | 1.18 |
| 20:00 | 1216 | Besiktas vs Yeni Malatyaspor | 1.35 | 4.92 | 7.68 |
| 20:00 | 2069 | Manisa BBSK vs Erzurum BB | 1.55 | 3.97 | 5.04 |
| 20:00 | 3150 | Kayserispor vs Kasimpasa | 2.62 | 3.21 | 2.62 |
| 20:00 | 5314 | Adanaspor vs Menemen Bld | 2.23 | 3.25 | 2.96 |
| 20:00 | 5627 | Santa Clara vs Benfica | 5.69 | 4.22 | 1.51 |
| 20:30 | 5530 | Panathinaikos vs Apollon Smyrnis | 1.44 | 4.22 | 6.87 |
| 21:00 | 1900 | Al Hala Muharraq vs Najma Manama | 3.96 | 3.38 | 1.83 |
| 21:00 | 4640 | Red Star Belgrade vs Proleter | 1.07 | 8.71 | 20.32 |
| 21:15 | 3645 | NK Mura vs Olimpija Ljubljana | 2.28 | 3.15 | 2.96 |
| 21:30 | 1715 | BSC Young Boys vs FC Zurich | 1.46 | 4.64 | 5.72 |
| 21:30 | 3013 | Longford Town vs Dundalk FC | 6.02 | 3.98 | 1.48 |
| 21:45 | 4584 | Atalanta vs Fiorentina | 1.58 | 4.31 | 5.21 |
| 22:00 | 3122 | AZ Alkmaar vs PSV Eindhoven | 3.05 | 3.64 | 2.12 |
| 22:00 | 5423 | Athletic Bilbao vs Mallorca | 1.71 | 3.61 | 5.22 |
| 22:00 | 5560 | Monaco vs Marseille | 2.03 | 3.54 | 3.44 |
| 22:30 | 4704 | Sporting Lisbon vs Porto | 2.52 | 3.11 | 2.81 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.






# MAN UNITED YAMKOMALIA RICE

**ESTER,** England

KLABU ya Manchester United, imeamua kuendelea kumkomalia kiungo mkabaji wa West Ham United, Declan Rice, kwa ajili ya kumsajili msimu ujao, licha ya timu yake kumwekea vikwazo katika dirisha kubwa la usajili lililopita.

Ikumbukwe kuwa, Rice alikuwa akihitajika pia na Chelsea wakati wa dirisha kubwa la usajili lililofungwa mwezi uliopita, lakini kwa Man United inaelezwa kwamba wameamua kusimamia katika uamuzi wa kumwinda kiungo huyo kwa ajili ya kuinasa saini yake msimu ujao.

Taarifa za ndani kutoka Manchester zinaeleza kuwa, katika dirisha hili lililofungwa Agosti 31, mwaka huu, United ilikuwa na vipaumbele vikuu viwili ambapo ilikuwa ni kusajili winga na beki mmoja.

Walifanikiwa kumsajili Jadon Sancho, anayecheza winga akitokea Borussia Dortmund kwa dau la euro milioni 85 na beki wa kati Mfaransa, Raphael Varane, kutoka Real Madrid kwa dau la euro milioni 40, huku pia ikimtwaa Cristiano Ronaldo kutoka Juventus.

Rice anatajwa kuwa kwenye orodha ya wachezaji ambao United wanatarajia kuwanasa msimu ujao, licha ya kuwa mhimili mkubwa kwenye kikosi cha Kocha Mkuu wa West Ham United, David Moyes, ambaye ana matumaini ya kuendelea kumtumia kwenye michuano ya Ligi ya Europa.

# *Mesut Ozil ataka kuondoka Fenerbahce*

**INSTANBUL,** Uturuki

NYOTA Mesut Ozil anasemekana kuwa hana furaha katika klabu ya Fenerbahce, miezi minane tu baada ya kujiunga na klabu hiyo ya Uturuki akitokea Arsenal.

Ozil mwenye umri wa miaka 32, alihamia Fenerbahce yenye makao yake Istanbul Januari mwaka huu akiwa mchezaji huru baada ya Arsenal kukubali kuvunja miezi sita ya mwisho ya mkataba wake kuokoa mshahara wa pauni 350,000 kwa wiki.

Gazeti la Hispania, Diario AS limesema kiungo huyo anataka kuondoka Fenerbahce licha ya kubakiza miaka mitatu kwenye mkataba wake wa sasa.

Hali hiyo imejitokeza licha ya Ozil kutamka alipowasili Istanbul kuwa: "Siku zote nilikuwa shabiki wa Fenerbahce, hii ni kutimia kwa ndoto yangu."

Lakini sasa nyota huyo wa Ujerumani ameonyesha wazi nia yake ya kutaka kuondoka nchini Uturuki.



# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# MESSI AVUNJA REKODI YA PELE

●●● Niliota kuhusu hili siku moja na shukrani kwa Mungu mambo yamekuwa sawa...

**BUENOS AIRES,** Argentina

LIONEL Messi ameipiku rekodi ya Pele kama mfungaji mwenye mabao mengi zaidi kwa bara la Amerika Kusini kwa kufunga 'hat-trick' wakati Argentina ikiibuka na ushindi dhidi ya Bolivia katika mchezo wa kufuzu Kombe la Dunia, juzi.

Akifunga mabao yote kwenye ushindi wa 3-0 mjini Buenos Aires, kumemfanya Messi kufikisha mabao 79 aliyoifungia Argentina katika mechi 153.

Gwiji wa Brazil, Pele alimaliza kipindi chake cha uchezaji kwa kufunga mabao 77 katika mechi 92.

**Bao la kwanza la Messi dakika ya 14 likamfanya kufikia rekodi ya Pele na kisha akaivunja kipindi cha pili.**

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 34, alifunga bao la pili kwa kumpiga chenga mlinzi na kisha kukamilisha hat-trick dakika mbili kabla ya mchezo kumalizika.

Baada ya mchezo, nahodha huyo wa Argentina, Messi na wachezaji wenzake walisherehekea wakiwa na Kombe la Copa America mbele ya mashabiki 20,000 kwenye Uwanja wa Monumental. Alikiongoza kikosi hicho kwenye taji lake la kwanza la kimataifa Julai wakati walipoifunga Brazil kwenye fainali.

"Niliota kuhusu hili siku moja na shukrani kwa Mungu mambo yamekuwa sawa," aliandika Messi kwenye ukurasa wake wa Instagram akiweka picha ya kombe hilo.

"Sina maneno mengi ya kuzungumza, asanteni sana wote kwa mapenzi mliyoonyesha. Ulikuwa usiku mzuri, nimefurahia sana, na nimefurahia sana."

## ZISIKUPITE

### KOUNDE KUSAJILIWA JANUARI

CHELSEA wamepanga kufufua ari yao kumsajili beki wa kati wa Ufaransa, Jules Kounde, 22, wakati wa dirisha la uhamisho la Januari ikiwa Sevilla itapunguza gharama yake kwa karibu euro milioni 50. ***(ESPN)***

### KESSIE AGOMBEWA ULAYA

KLABU za Chelsea, Paris St-Germain na Liverpool, pia zinasemekana kumtaka kiungo wa kati wa AC Milan na Ivory Coast, Franck Kessie, 24. ***(Calciomercato)***

### EN-NESYRI ATAJWA ARSENAL

ARSENAL wameripotiwa kumtambua mshambuliaji wa Sevilla, Youssef En-Nesyri, 24, kama mbadala bora wa muda mrefu wa mshambuliaji wa Gabon, Pierre-Emerick Aubameyang. ***(La Colina de Nervion)***

### COMAN HATAKI MKATABA

WINGA wa Bayern Munich, Kingsley Coman, huenda akakataa ofa zozote kutoka kwa mabingwa hao wa Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, ili kuongeza mkataba mpya, kwani anafikiri kwenye Ligi Kuu England. ***(Le10Sport - in French)***

### TIELEMANS AMULIKWA ULAYA

KIUNGO wa Ubelgiji, Youri Tielemans, 24, anatazamwa na Real Madrid, Barcelona na Manchester United wakati Leicester ikijaribu kumfunga nyota huyo kwa mkataba mpya. ***(AS - in Spanish)***

### LEICESTER YAMTAKA BERARDI

LEICESTER pia wamewasiliana na Sassuolo ya Ligi Kuu Italia, Serie A, kuhusu winga wa Italia, Domenico Berardi, 27, juu ya uwezekano wa uhamisho wa Januari ***(Leicester Mercury)***

### BARCA NA OFA KWA NEYMAR

BARCELONA ilitoa ofa ya pauni milioni 68 kumsajili tena mshambuliaji, Neymar, 29, kabla ya ukweli wa shida za kifedha za klabu hiyo kushuhudia Lionel Messi akihama na kujiunga na Paris St-Germain. ***(Star)***

### SOLER AWANIWA LIVERPOOL

LIVERPOOL itamlenga kiungo wa Valencia na Hispania, Carlos Soler, 24, kama mbadala wa Georginio Wijnaldum, 30, ambaye aliondoka kujiunga na PSG msimu huu wa majira ya joto. ***(Fichajes)***

### POGBA AISHAURI UNITED

KIUNGO wa kati wa Manchester United na Ufaransa, Paul Pogba, anadhani kocha Ole Gunnar Solskjaer anapaswa kumsajili kiungo wa Ufaransa anayeichezea Monaco, Aurelien Tchouameni, 21. ***(Express)***

### MAITLAND-NILES KUBAKI

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta anafurahi Ainsley Maitland-Niles, 22, atabaki na alifichua kuwa alifanya mazungumzo ya faragha na kijana huyo baada ya kiungo huyo wa England kuelezea hadharani hamu ya kuondoka klabuni hapo majira haya ya joto. ***(Mirror)***

# HABARI MICHEZO

## Ufaransa yageukia wasanii kutangaza utamaduni Afrika

**Na Gwamaka Alipipi**

UBALOZI wa Ufaransa nchini, umeanzisha programu maalum inayowakutanisha wasanii kutoka nchi mbalimbali Afrika kwa ajili ya kufanya sanaa za maonyesho kuwainua wanawake, pamoja na kutangaza utamaduni wa jamii za kiafrika.

Akizungumza na waandishi wa habari wakati wa uzinduzi wa programu hiyo jijini Dar es Salaam jana, Kaimu Katibu Mkuu wa Baraza la Sanaa la Taifa (BASATA), Mniko Matiko, alisema uzinduzi huo ni hatua kubwa itakayowawezesha wasanii wa Tanzania kuitangaza nchi pamoja na kutangaza vipaji vyao kimataifa.

Matiko alisema: "Hii ni hatua kubwa katika kukuza utamaduni wa kiafrika, wasanii wetu watakuwa na nafasi ya kubadilishana mawazo pamoja na maarifa ya wasanii wenzao kutoka mataifa mbalimbali".

Alisema serikali itahakikisha inashirikiana na wasanii kuhakikisha programu hiyo inafanikiwa na kuleta manufaa kwa Taifa na wasanii kwa ujumla. Matiko alisema kwa kuanza kuitangaza programu hiyo hapa nchini itaanza katika mikoa ya Arusha, baadaye Dar es Salaam kisha kumalizia visiwani Zanzibar.

Naye Mtunzi na Mwandaaji wa maigizo ya programu hiyo kutoka Msumbiji, Alain Martial, akizungumza wakati wa uzinduzi huo alisema dhumuni la kuanzishwa kwa tamasha hilo lililopewa jina la 'Genesis' ni kutangaza tamaduni za Afrika, pamoja na mila za mataifa mbalimbal ikiwamo Tanzania, Kenya, Uganda, Msumbiji na visiwa vya Comoro.

## TTA kusaka timu ya Taifa ya Wanaume

**Na Shufaa Lyimo**

CHAMA cha Mchezo wa Tenisi Tanzania (TTA), kimesema kwa sasa kinaendelea na mchakato wa kusaka vipaji kwa ajili ya kuunda timu ya Taifa ya Wanaume, inayotarajiwa kushiriki mashindano ya dunia mwakani.

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam juzi, Mwenyekiti wa TTA, Denis Makoi, alisema awali walifanikiwa kupata timu ya Taifa ya Wanawake na sasa mchakato unaofuata ni wa kusaka timu ya wanaume ambao unatarajiwa kufanyika jijini Arusha mwezi ujao.

"Kwa sasa tupo kwenye mchakato wa kutafuta timu ya Taifa ya Wanaume kwa ajili ya kujiandaa kushiriki mashindano ya dunia, zoezi hilo litafanyika mwezi ujao. Kwa upande wa timu ya Wanawake tayari tumepata kwa sasa wanaendelea kufanya mazoezi," alisema Makoi.

Mwenyekiti huyo alisema kwa upande wa Tanzania ni mara ya kwanza kwenda kushiriki mashindano makubwa kama hayo, hivyo wanawapa mbinu wachezaji wao kwa kuangalia jinsi nchi nyingine zinavyofanya kwenye mashindano ya miaka iliyopita.

# BMT YATOA MWONGOZO UAGIZAJI NYASI BANDIA

**Na Saada Akida**

BARAZA la Michezo la Taifa (BMT), imetoa taratibu za maombi ya kuondolewa gharama za kodi za nyasi bandia zitakazoagizwa hapa nchini kutoka nje kwa ajili ya maboresho ya viwanja vya soka Tanzania.

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, Ofisa Uhusiano wa BMT, Najaha Bakari, alisema baada ya awali kuwapo kwa changamoto ya gharama ya kuingizwa kwa nyasi bandia nchini kutokana na kodi ya forodha na ile ya ongezeko la thamani (VAT), serikali ilisikia kilio hicho na kutafuta suluhisho kwa kufuta VAT, lakini kuna taratibu ambazo zinapaswa kufuatwa kabla ya kuziagiza.

"Tumeweka utaratibu wa maombi ili kuondolewa kwa kodi ya nyasi bandia zinazoagizwa [kuainisha] gharama za nyasi, mfanyabiashara, chama, shirikisho ama mwekezaji atapaswa kutuma maombi ya kuondolewa VAT kwa kuandia barua kwenda kwa Katibu Mtendaji wa BMT.

**"Baraza litaridhia na kuidhinisha maombi yatakayokidhi vigezo vilivyoainishwa katika mwongozo, na nyasi zitakazopata idhini ya msamaha wa kodi ni zile zitakazotumika kwenye viwanja vya michezo wa mpira wa miguu," alisema Najaha.**

Aidha, alisema mwombaji wa msamaha wa kodi za nyasi bandia, anapaswa kutuma maombi ya msamaha wa kodi baada ya kukamilisha ununuzi wa nyasi hizo.

Najaha alisema BMT itachambua na kuchakata maombi hayo na yatakayoridhiwa yatapelekwa Wizara ya Fedha na Mipango ili kupata idhini ya msamaha wa kodi.

Alitaja sifa za mnufaika wa msamaha wa kodi wa nyasi bandia kwamba muombaji anaweza kuwa taasisi, shirikisho, chama au mtu binafsi anayeomba kwa niaba ya taasisi awasilishe nyaraka ya kumtabulisha kutoka mamlaka husika.

"BMT itafanya ukaguzi wa kiwanja kitakachowekwa nyasi bandia ambazo zinaombewa msamaha wa kodi kabla ya kibali kutolewa," alisema Najaha.

**TAMADUNI...**



Kaimu Mtendaji Mkuu wa Baraza la Sanaa la Taifa (Basata), Matiko Mniko (kulia), akizungumza jijini Dar es Salaam jana wakati wa Uzinduzi wa Tamasha la Kitamaduni linalojumuisha wasanii kutoka nchi za Afrika Mashariki na Kusini, lengo likiwa ni kudumisha tamaduni za kiafrika. Kushoto ni Mwandishi wa Maigizo, Alain Kamal na katikati ni msanii kutoka Kenya, Mammito Eunice. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *KMKM yatamba kuwafumua Walibya michuano ya CAF leo*

**Na Hawa Abdallah**, ZANZIBAR

WAKATI KMKM ikishuka dimbani leo kuikaribisha Al-Ittihad ya Libya kwenye mechi Ligi ya Mabingwa Afrika, Kocha Mkuu wa mabingwa hao wa Zanzibar, Ali Vuai Shein, amesema kikosi chake kimejipanga vizuri kuibuka na ushindi mnono ili kujiwekea mazingira mazuri ya kusonga mbele katika michuano hiyo inayoongoza kwa utajiri kwa ngazi ya klabu barani Afrika.

KMKM leo itashuka Uwanja wa Amaan kuwavaa mabingwa hao wa Libya katika mchezo wa raundi ya awali ya michuano hiyo ya Afrika kwa ngazi ya klabu.

Akizungumza katika mkutano na waandishi wa habari jana, ambao wapinzani wao, Al-Ittihad hawakuhudhuria, Shein alisema timu yake imefanya maandalizi mazuri kuelekea michuano hiyo licha ya kutopata mechi ya kirafiki dhidi ya timu kutoka nje ya Zanzibar kujipima uwezo.

Alisema wana uzoefu wa kutosha kwenye michuano hiyo na tofauti kwao itakuwa ni mara ya kwanza kukutana na timu hiyo kutoka Libya katika hatua hii, lakini hali hiyo haiwezi kuwa kikwazo kwao cha kushindwa kutimiza lengo lao la ushindi.

"Tuna uzoefu na michuano hii ya kimataifa, kikubwa ni wachezaji wetu kuondoa hofu ya mchezo pamoja na kuweka mbele malengo ya kushinda kuliko kupoteza, hii itatusaidia," alisema.

Aidha, alisema kupitia michuano ya CECAFA iliyomalizika hivi karibuni, imemsaidia kuwaondoa hofu wachezaji wake kuelekea mashindano hayo ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Michezo
Jumamosi Septemba 11, 2021
Nipashe



Messi avunja rekodi ya Pele UKURASA 22

# Hitimana Kocha Mkuu Simba CAF, Gomes msaidizi

● ● ● Asaini rasmi mwaka 1...

**Na Saada Akida**

BAADA ya Shirikisho la Soka barani Afrika (CAF), kutaja orodha ya makocha ambao hawana sifa ya kuziongoza timu zao kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho Afrika kuanzia msimu huu, huku Kocha Mkuu wa Simba, Mfaransa Didier Gomes, akiwa miongoni mwao, haraka klabu hiyo imechukua hatua stahiki kufanikiwa kumrejesha katika benchi la timu hiyo, imefahamika.

**CAF juzi ilitangaza kuwa kuanzia msimu huu kocha mkuu anapaswa kuwa na Leseni ya UEFA A Pro ambayo ni sawa na Caf A, huku makocha wasaidizi wakipaswa kuwa na Leseni B, jambo ambalo makocha wote wa Simba, Kocha Mkuu, Gomes anakosa sifa hiyo huku pia Msaidizi wake, Selemani Matola naye akikosa sifa katika nafasi yake.**

Hata hivyo, haraka bila kupoteza muda uongozi wa Klabu ya Simba ukaonyesha umakini wake kwa kuhakikisha inafanya mazungumzo na kumsainisha Thierry Hitimana mkataba wa mwaka mmoja ili kuja kusimama kama kocha mkuu wa timu hiyo kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika wakati Gomes atakuwa akibeba jukumu la kocha msaidizi.

Gomes ambaye leseni yake ni UEFA Diploma A, daraja hilo linamruhusu kuwa kocha msaidizi katika michuano hiyo ya CAF, lakini kwa upande wa Ligi Kuu anakidhi vigezo vya kuwa kocha mkuu, hivyo katika mechi za ndani ataendelea na jukumu lake la ukocha mkuu ambapo sasa atakuwa akisaidiwa na Hitimana pamoja na Matola.

Hitimana mwenye Leseni A ya CAF, daraja ambalo linamruhusu kuwa kocha mkuu kwenye michuano ya shirikisho hilo na mingine nchini, alikuwa asaini mkataba na Mtibwa Sugar, lakini jana aliikacha ofa hiyo na kwenda kumwaga wino Simba baada ya kutangaziwa dau nono zaidi.

Sheria mpya ambayo inaanza msimu huu inataka kocha ambaye anatoka ndani ya Afrika lazima awe na Leseni ya CAF A na kwa makocha ambao wanatoka nje ya Afrika kwa Bara la Ulaya wawe na Uefa A Pro.

Taarifa za uhakika zilizolifikia gazeti hili jijini jana kutoka chanzo chetu ndani ya Bodi ya Wakurugenzi wa Simba, tayari klabu hiyo imemalizana na Hitimana, ambaye anakidhi vigezo vya kuwa na leseni ya CAF A, na sasa atakuwa akisaidiwa na Gomes kwenye michuano hiyo ya kimataifa.

"Katika kuimarisha benchi la ufundi, tumempa mkataba wa mwaka mmoja kwa ajili ya kusaidiana na Gomes na Matola, kuelekea michuano ya kimataifa," alisema mjumbe mmoja kutoka kwenye bodi hiyo ambaye hakutaka jina lake litajwe kwa kuwa si msemaji katika suala hilo.

Gazeti hili lilimtafuta Hitimana, ambaye alikiri kumalizana na uongozi wa Simba kwa mkataba wa mwaka mmoja kwenda kuwa sehemu ya benchi la ufundi la timu hiyo kwa msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara na michuano ya kimataifa.

"Ni kweli nilikuwa na mazungumzo na viongozi wa Simba na tayari nimesaini mwaka mmoja, makubaliano mengi ni baada ya nusu msimu tutakaa na kuzungumza kuhusu kuongeza mkataba mwingine," alisema Hitimana.

Kuhusu Mtibwa Sugar, alisema hadi anarejea Tanzania, alikuwa na makubaliano ya kuja kuinoa timu hiyo, lakini Simba wamefanikiwa kumpa ofa nzuri ambayo imezidi ile ya mwajiri wake wa zamani, 'Wakata Miwa' hao.

Kwa upande wa Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Habari na Mawasiliano Simba, Ezekiel Kamwaga, alisema: "Tulishajua na si suala la 'suprise' kwetu, tumejiandaa vizuri na tunawahakikishia mashabiki wa Simba wasubiri hadi Januari na Kocha Gomes atakuwa sehemu ya benchi la ufundi la Simba".



Hitimana. **PICHA: MAKTABA YETU**

## Simba, Yanga Desemba 11 Ligi Kuu Bara

**Na Saada Akida**

BODI ya Ligi Tanzania (TPLB), imetangaza Ratiba ya Ligi Kuu Bara msimu wa 2021/22, huku mchezo wa watani wa jadi, ukipangwa kupigwa Desemba 11, mwaka huu katika Uwanja Benjamin Mkapa, mechi ambayo Simba itakuwa mwenyeji.

Ligi Kuu msimu huu itakuwa na jumla ya michezo 240, timu zikiwa 16 tofauti na mwaka uliopita ambapo kulikuwa na michezo 306 huku kila timu ikicheza jumla ya michezo 18 nyumbani na idadi kama hiyo ugenini.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Mtendaji Mkuu wa TPLB, Almasi Kasongo, alisema ratiba ya msimu huu imezingatia mapumziko ya michezo ya kimataifa, Kombe la Shirikisho na Mapinduzi Cup.

"Msimu huu kuna Kalenda 19 za michezo ya Shirikisho la Soka Afrika (CAF) na Fifa, lakini kuna mashindano ya Mapinduzi ambayo mara nyingi ilikuwa ikiharibu ratiba yetu. Pia kuna michezo imegawanyika katika makundi tofauti kuna itakayochezwa saa nane mchana ambayo itakuwa 31, mechi za saa 10 zitakuwa 125 na zitakayochezwa saa 11 itakuwa miwili.

"Pia michezo 12 itakuwa tisa, saa moja jioni itakuwa mechi 57 na saa mbili zitachezwa michezo nane wakati huo huo michezo nane bado haijapangiwa ratiba," alisema Kasongo.

Alisema kuwa Ligi Kuu itachezwa katikati ya wiki na mwisho wa wiki na raundi ya kwanza itachezwa Septemba 27, utakuwa mchezo baina ya Mtibwa Sugar dhidi ya Mbeya Kwanza utakaochezwa saa nane mchana. Michezo mingine ya ufunguzi Namungo dhidi ya Geita saa 10:00 jioni na Coastal Union dhidi Azam.

Septemba 28, Dodoma Jiji na Ruvu Shoting, Mbeya City dhidi ya Tanzania Prisons, Biashara United dhidi ya Simba Karume Mara, Polisi Tanzania dhidi ya Kmc huku Kagera Sugar ikiialika Yanga. Kwa mujibu wa ratiba, ligi hiyo inatarajiwa kumalizika Juni 19, mwakani.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P [illegible]

9 770856 541002 >